TANGAZO LA SERIKALI NA. 679 la tarehe 9/8/2024

SHERIA YA UMEME
(SURA YA 131)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 22(1) na 45(a))*

## KANUNI ZA SHUGHULI ZA UZALISHAJI, USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI UMEME ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TARATIBU ZA UTOAJI LESENI

4. Wajibu wa kuomba leseni.
5. Taratibu za kuomba leseni.
6. Kutangaza ombi la leseni.
7. Kutoa leseni.
8. ombi la leseni ya muda mfupi.
9. Kutangaza ombi la leseni ya muda mfupi.
10. Kutoa leseni ya muda mfupi.
11. Msamaha.
12. Kutangaza ombi la kuomba msamaha.
13. Kutoa msamaha.
14. Sababu za maamuzi.
15. Taratibu za rufaa.
16. Muda na uhamisho wa leseni.
17. Kusitisha na kufuta leseni.

SEHEMU YA TATU
WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI

18. Mmiliki wa leseni ya uzalishaji.
19. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji.
20. Mmiliki wa leseni ya usambazaji.
21. Mmiliki wa leseni ya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi.
22. Wajibu wa jumla wa mmiliki wa leseni.
23. Mkataba wa huduma kwa mteja.
24. Fidia kwa hasara iliyopatikana.
25. Taarifa za mwaka.
26. Taarifa ya utendaji.
27. Ukaguzi wa uzingatiaji.
28. Mpango wa kuboresha utendaji.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA KIFEDHA

29. Utoaji wa taarifa za kifedha.
Viwango vya utoaji wa taarifa za kifedha.
30. Utunzaji wa akaunti tofauti.
31. Zuio la mwingiliano wa ruzuku.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA KIUFUNDI

*Sehemu Ndogo ya Kwanza*
*Wajibu wa Kiufundi wa Mmiliki wa Leseni ya Uzalishaji*

32. Mpango wa usitishaji huduma na matengenezo kinga.
33. Katizo la huduma na matengezezo ya dharura.
34. Taarifa ya Katizo la huduma.
35. Uhakika Wa Ugavi.
36. Upimaji.
37. Majaribio na Uhakiki.

*Sehemu Ndogo ya Pili*
*Wajibu wa Kiufundi wa Mmiliki wa Leseni ya Usafirishaji*

38. Ruhusa na ofa ya kujiunga au kutoa huduma ya usafirishaji.
39. Wajibu wa jumla wa mmiliki wa leseni ya usafirishaji.

40. Haki za mmiliki wa leseni ya usafirishaji.
41. Taarifa ya utendaji wa miundombinu ya usafirishaji.
42. Mpango wa miundombinu ya usafirishaji na utwaaji wa ardhi.
43. Mpango wa upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji.
44. uwiano wa nguvu za umeme.
45. Upotevu wa umeme kwenye mfumo wa usafirishaji.
46. Kuzingatia maelekezo ya mwendeshaji wa mfumo na soko.
47. Kuwasilisha taarifa kwa mwendeshaji wa mfumo na soko.
48. Maandalizi ya kukabiliana na dharura.
49. Matengenezo ya kawaida.
50. Matengenezo ya dharura na ukarabati.
51. Matengenezo Kinga.
52. Katizo la huduma lililopangwa.
53. Katizo la umeme lisilopangwa.
54. Notisi ya katizo la huduma.
55. Meta.
56. Mpango wa kuboresha utendaji.
57. Mpango wa kuhakiki ubora.

*Sehemu Ndogo ya Tatu*
*Wajibu wa Kiufundi wa Mmiliki wa Leseni ya Usambazaji*

58. Ruhusa na ofa ya kujiunga au kutoa huduma ya usambazaji.
59. Mkataba wa ugavi.
60. Mpango wa miundombinu ya usambazaji na utwaaji wa ardhi.
61. Makadirio ya matumizi.
62. Uhakika na usalama wa ugavi.
63. Ubora wa huduma.
64. Uwiano wa nguvu za umeme.
65. Upotevu wa umeme kwenye mfumo wa usambazaji.
66. Maandalizi ya kukabiliana na dharura.
67. Mpango wa usitishaji umeme kwa ajili ya matenegezo kinga.
68. Katizo la huduima na matengenezo ya dharura.
69. Taarifa ya katizo la huduma ya usambazaji.
70. Upimaji.
71. Kugundua na kuzuia wizi, uharibifu na kuchezea mita.
72. Mpango wa kuboresha utendaji.

SEHEMU YA SITA
UTAMBUZI WA WATEJA MAALUM

73. Maombi ya kuwa mteja maalum.
74. Vigezo kuwa mteja maalum.
75. Haki za mteja maalum.
76. Nguvu ya masharti haya.

SEHEMU YA SABA
UFUATILIAJI NA UTEKELEZAJI

77. Ukaguzi.
78. Wajibu wa Mkaguzi wakati wa ukaguzi.
79. Vitendo vilivyokatazwa kwa Mkaguzi.

SEHEMU YA NANE
USIMAMIZI WA CHUMBA CHA UDHIBITI

80. Mahitaji ya jumla.
81. Wajibu.
82. Taratibu.
83. Kuzingatia utaratibu wa dharura.
84. Majukumu na wajibu.
85. Taarifa inayotosheleza.
86. Kuhimili uchovu.
87. usimamizi wa kiashirio.
88. Uhakiki wa SCADA.
89. Usimamizi wa mabadiliko.
90. Uzoefu wa uendeshaji.
91. Mpangilio wa chumba cha udhibiti.
92. Hali ya joto.
93. Muonekano.
94. Hali ya usikivu.
95. Kiashiria.
96. Lugha.
97. Lebo.
98. Vifaa vya kuonesha.
99. Uhakiki wa mazingatio.
100. Uzingatiaji na ukiukaji.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

101. Mpango wa kuondoa miundoimbinu.
102. Kuondoa miundombinu leseni inapofutwa.
103. Makosa.
104. Kufutwa kwa Kanuni.

---

JEDWALI

---

SHERIA YA UMEME,
(SURA YA 131)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 21(4) na 45)*

KANUNI ZA SHUGHULI ZA UZALISHAJI, USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme, za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kusimamia masuala ya udhibiti wa shughuli zinazohusiana na-

(a) uzalishaji wa umeme ikijumuisha uzalishaji kwa matumizi binafsi, usafirishaji, usambazaji na biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi;
(b) wateja maalum; na
(c) usimamizi wa chumba cha udhibiti.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura ya 131

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Umeme;

"mshirika" maana yake ni chombo chochote cha kisheria chenye hisa kwa mmiliki wa leseni au chombo cha kisheria kingine ambacho mmiliki wa leseni ni mbia;

"kiashiria" maana yake ni mfumo unaosikika au unaoonekana unaompa tahadhali mwendeshaji wa chumba cha udhibiti kuwa kifaa, au mfumo wa uendeshaji una kasoro na ni hatari kulingana na vigezo vya usalama;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

Sura ya 414

"biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi" maana yake ni biashara ya umeme kati ya nchi mbili zinazopakana

kupitia kiunganishi cha umeme, au biashara kati ya nchi mbili zisizokuwa na mipaka ya pamoja, lakini zinaunganishwa kupitia mtandao wa umeme unaohusisha usafirishaji wa nishati ya umeme kati ya nchi husika;

"leseni ya kufanya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi" maana yake ni leseni inayotolewa na Mamlaka kwa mtu kwa lengo la kumuwezesha kufanya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi;

"chumba cha udhibiti" maana yake ni kituo cha uendeshaji chenye wafanyakazi wenye jukumu la kufuatilia na kudhibiti mfumo wote au vitengo vingi vya miundombinu ya umeme;

"mwendeshaji wa chumba cha udhibiti " maana yake ni mtu mwenye sifa stahiki mwenye jukumu la kufuatilia na kudhibiti usalama wa mfumo wote au vitengo vingi vya miundombinu ya umeme kupitia SCADA iliyofungwa ndani ya chumba cha udhibiti na ambaye ana mamlaka ya uendeshaji na anawajibika na majukumu ya kila siku ya kufuatilia uendeshaji wa miundombinu ya umeme kama itakavyoelekezwa na mmiliki wa leseni;

"mteja" maana yake ni mtu anayepokea au anayenunua huduma zinazodhibitiwa kutoka kwa mmiliki wa leseni;

"kanuni za usambazaji" maana yake ni kanuni na viwango vya kiufundi na kiutaratibu vinavyotolewa na Mamlaka vinavyosimamia masuala yanayohusu usambazaji wa umeme;

"leseni ya usambazaji" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa ajili ya kuendesha mtandao wa usambazaji;

"mmiliki wa leseni ya usambazaji" maana yake ni mtu aliyepewa leseni ya kuendesha mtandao wa usambazaji na Mamlaka na inajumuisha mtu iliyesamehewa kuwa na leseni ya usambazaji kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria;

"mtandao wa usambazaji" maana yake ni miundombinu na vifaa vya mmiliki wa leseni ya usambazaji vilivyoundwa kwa ajili ya kusambaza umeme usiozidi msongo wa kilovolti 33 ambayo inajumuisha njia za

juu, nyaya za ardhini, mashine umba, vituo vya udhibiti na vifaa vya kupima matumizi umeme;

"mteja maalum" maana yake ni mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mamlaka kwa mujibu wa kanuni hizi kuingia katika mkataba wa kununua umeme moja kwa moja kutoka kwa mmiliki wa leseni ya uzalishaji;

"kituo" maana yake ni eneo au miundombinu ya umeme iliyojengwa na inakidhi viwango vya kimataifa ikijumuisha uzalishaji umeme, usafirishaji, usambazaji na mfumo wa kushughulikia majanga ya moto wakati shughuli inayodhibitiwa inatekelezwa;

"kituo cha vifaa vya uzalishaji" maana yake ni majengo, vifaa vya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na vifaa saidizi, mashine-umba, vifaa vya kushughulikia mafuta, mtambo wa kubadilishia umeme na kiunganishia umeme ambavyo ni muhimu kwa shughuli za kuzalisha umeme kama zitakavyoelezwa kwenye leseni ya kuzalisha umeme;

"uzalishaji kwa matumizi binafsi" maana yake ni kuzalisha umeme ambao wote utatumiwa na mmiliki wa leseni pasipo kusambaza kwa mtu mwingine;

"leseni ya uzalishaji" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa ajili ya shughuli za uzalishaji;

"mmiliki wa leseni ya uzalishaji" maana yake ni mtu aliyepewa leseni na Mamlaka kwa ajili ya kutoa huduma za uzalishaji na inajumuisha mtu yeyote aliyesamehewa kupata leseni ya uzalishaji kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria;

"huduma za uzalishaji" maana yake ni huduma za uzalishaji umeme ikiwa ni pamoja na kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi na maneno "shughuli ya kuzalisha umeme" yatatafsiriwa kwa namna hiyo;

"kanuni za gridi" maana yake ni kanuni na viwango vya kiufundi na kiutaratibu vinavyotolewa na Mamlaka kwa ajili ya usafirishaji na uendeshaji wa mfumo;

"mkaguzi" maana yake ni afisa wa Mamlaka au wakala aliyeteuliwa na Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 31(2) cha Sheria kuwa mkaguzi;

"kituo cha kuunganisha" maana yake ni kituo ambacho kinapokea umeme kutoka katika kituo cha uzalishaji na kuingiza kwenye njia za usambazaji au usafirishaji

wa umeme;

"barua ya kuonesha nia " maana yake ni andiko la nia kutoka kwa mmiliki was leseni ya usambazaji ya kuridhia kuunganisha na kununua umeme wa mpaka megawati 10 utakaozalishwa na mwekezaji;

“leseni” maana yake ni leseni ya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi, leseni ya uzalishaji, leseni ya usafirishaji umeme au leseni ya usambazaji umeme iliyotolewa na Mamlaka;

“mmiliki wa leseni” maana yake ni mmiliki wa leseni ya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi, leseni ya uzalishaji umeme, leseni ya usafirishaji umeme au leseni ya usambazaji umeme;

"kituo kilichopewa leseni" maana yake ni majengo na vifaa vya kuzalisha, kusafirisha au kusambaza nishati ya umeme ikijumuisha vifaa visaidizi, mashine umba, vifaa vya kutunzia mafuta, sehemu ya kuzima na kuwasha umeme na viunganishi ambavyo ni muhimu kwa ajili ya kutekeleza shughuli inayodhibitiwa kama ilivyoainishwa katika leseni husika;

Sura ya 287 na 288

“mamlaka ya serikali ya mtaa” maana yake ni mamlaka ya wilaya, mamlaka ya miji, mamlaka ya kata au mamlaka ya kijiji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

Sura za 287 na 288

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya umeme;

“mkataba wa ununuzi wa umeme” maana yake ni mkataba wa kuuza au kununua umeme ulioingiwa kati ya mmiliki wa leseni ya uzalishaji na mtu mwingine yeyote;

“leseni ya muda mfupi” maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kumruhusu mwombaji kufanya matayarisho ya shughuli mbalimbali kama uchunguzi, utafiti na shughuli nyingine muhimu kwa ajili ya kuomba leseni;

“Matendo Bora ya Utoaji Huduma" ina maana ya matendo mazuri na bora, mbinu na utaratibu ambao unapatikana kwa kutumia ujuzi, bidii, busara na kubashiri yaliyo mbeleni ambayo kwa kawaida yanatarajiwa kupatikana kutoka kwa mtaalam

mbobezi wa kimataifa anayefanya kazi hizo au shughuli inayofanana na inayodhibitiwa ndani ya Tanzania na ambayo iko chini ya mazingira yanayofanana na yanakidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa ya kiafya, usalama na mazingira;

"shughuli inayodhibitiwa" maana yake ni biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi, shughuli ya uzalishaji umeme, usafirishaji umeme au usambazaji umeme na maneno "huduma inayodhibitiwa" yatatafsiriwa kwa namna hiyo;

"taarifa za fedha za kiudhibiti" maana yake ni kumbukumbu za fedha au taarifa zilizotayarishwa na kuwasilishwa kwa Mamlaka na taasisi inayodhibitiwa kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa utoaji taarifa za fedha za taasisi zinazodhibitiwa;

"SCADA" maana yake ni mfumo unaotumia kompyuta au mfumo ambao unakusanya na kuonesha taarifa kuhusu miundombinu ya umeme na una uwezo wa kutuma maagizo kwenda kwenye miundombinu ya umeme au mfumo ambao unajumuisha vifaa vya kompyuta na programu inayotumiwa kupeleka maagizo na kupata takwimu kwa madhumuni ya kufuatilia na kudhibiti miundominu ya umeme;

"eneo" maana yake ni sehemu ambayo miundombinu ya uzalishaji imewekwa na maelezo yake yatatolewa kwenye leseni;

"mradi mdogo wa umeme" maana yake ni kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu au joto la ziada au mchanagnyiko wa vyote isiyozidii Megawati 10;

"bei" maana yake ni tozo yoyote, ada, au kiasi kwa madhumuni ya kununua huduma inayodhibitiwa kama itakavyoidhinishwa na Mamlaka;

"leseni ya usafirishaji" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa mmiliki wa leseni kwa ajili ya kuendesha mtandao wa usafirishaji;

"mbinu ya upangaji bei" maana yake ni njia inayotumika kupanga bei kama ilivyoidhinishwa na Mamlaka;

"leseni ya usafirishaji" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa ajili ya kuendesha mtandao wa usafirishaji;

"mmiliki wa leseni ya usafirishaji" maana yake ni mtu aliyepewa leseni na Mamlaka kwa ajili ya kuendesha mtandao wa usafirishaji na inajumuisha mtu yeyote aliyesamehewa kupata leseni ya usafirishaji kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria;

"mtandao wa usafirishaji" maana yake ni mkusanyiko wa vifaa na miundombinu ya umeme inayomilikiwa na mwenye leseni ya upelekaji umeme katika masafa ya hazi 50 *(50Hz)* kwa njia ya msongo wa juu wa kilovolti 66 au zaidi, ikijumuisha nyaya za juu, chini ya ardhi, chini ya maji, mashine umba, mtandao wa mawasiliano, vituo vya udhibiti na vifaa vya kupimia umeme;

"Mkataba wa kusafirisha umeme" maana yake ni mkataba wa usafirishaji umeme kutoka katika chanzo kilichounganishwa kwenye gridi ya umeme hadi kwa mtumiaji ndani ya gridi; na

"Msimamizi" maana yake ni mtu mwenye sifa za kufanya shughuli za ufilisi wa makampuni.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA KUOMBA LESENI

Wajibu wa kuomba leseni

4.-(1) Mtu hatafanya shughuli yoyote inayodhibitiwa bila kuwa na leseni.

(2) Mtu anayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Utaratibu wa maombi ya leseni

5.-(1) Mtu anayekusudia kufanya shughuli inayodhibitiwa ataomba leseni kwa Mamlaka kama itakavyoelekezwa na Mamlaka na maombi hayo yataambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) nakala zilizothibitishwa za nyaraka za usajili wa mwombaji ;
(b) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;
(c) vyeti vya usajili wa Utambulisho wa Mlipa Kodi na Kodi ya Ongezeko la Thamani;
(d) chanzo cha fedha za mradi;
(e) nakala ya cheti cha tathmini ya athari za

Sura ya 191

mazingira na jamii kwa ajili ya kituo kama inavyotakiwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

(f) taarifa nyingine yoyote inayohusiana na masuala ya kiudhibiti kama itakavyohitajika na Mamlaka.

(2) Pamoja na taarifa zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (1), maombi ya leseni yataambatana na:

(a) kwa leseni ya uzalishaji:
   (i) barua ya kuunga mkono maombi kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya umeme;
   (ii) uthibitisho wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;
   (iii) uthibitisho wa haki ya kutumia maji kwa waombaji wanaotaka kuzalisha umeme kwa kutumia maji;
   (iv) uthibitisho wa haki ya kutumia ardhi kwa ajili ya miundombinu ya umeme;
   (v) uthibitisho wa kibali cha kuendeleza eneo ikiwa ni pamoja na kibali cha ujenzi;
   (vi) taarifa ya upembuzi yakinifu;
   (vii) mkataba wa kuuziana umeme pale inapohitajika;
   (viii) ramani ya mpangilio wa matumizi ya eneo;
   (ix) maelezo ya kituo cha uzalishaji;
   (x) mchoro wa kituo kama kilivyojengwa;
   (xi) taarifa ya ukamilifu wa mradi;

(b) kwa leseni ya usafirishaji:
   (i) uthibitisho wa upatikanaji wa nishati ya umeme itakayosafirishwa ikijumuisha mkataba wa mauziano ya umeme, leseni ya kununua umeme kuingiza ndani ya nchi au mkataba wowote wa kutumia mfumo wa usafirishaji;
   (ii) maelezo ya eneo la huduma;
   (iii) maelezo ya mtandao wa usafirishaji;
   (iv) uthibitisho wa haki ya njia kwa ajili ya miundombinu;

(v) taarifa ya upembuzi yakinifu;
(vi) mpango wa upanuzi wa mtandao wa usafirishaji, kama upo;
(vii) mchoro wa mtandao wa usafirishaji kama ulivyojengwa; na
(viii) taarifa ya ukamilifu wa mradi;

(c) kwa leseni ya usambazaji:
(i) barua ya kuunga mkono maombi kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya umeme;
(ii) uthibitisho wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;
(iii) uthibitisho wa upatikanaji wa nishati ya umeme itakayosambazwa;
(iv) taarifa ya upembuzi yakinifu;
(v) maelezo ya eneo linalokusudiwa kusambaziwa huduma ;
(vi) maelezo ya mtandao wa usambazaji;
(vii) mpango wa upanuzi, kama upo;
(viii) mchoro wa mtandao wa usambazaji kama ulivyojengwa; na
(ix) taarifa ya ukamilifu wa mradi.;

(d) kwa biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi:
(i) mkataba wa mauziano ya umeme;
(ii) Mkataba wa uunganishwaji miundombinu;
(iii) mkataba baina ya nchi kama upo, na
(iv) mkataba wa kusafirisha umeme, pale utakapohitajika.

(3) Maombi ya leseni yataambana na ada ya maombi isiyorejeshwa itakayoainishwa na Mamlaka.

(4) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, maombi ya leseni ya usafirishaji yatafanywa na taasisi ya usafirishaji inayomilikiwa na Serikali.

Kutangaz wa kwa maombi ya leseni

6.-(1) Maombi ya leseni yaliyopokelewa na Mamlaka yatafanyiwa tathmini ili kujiridhisha na usahihi wake na uhalali wa taarifa zilizotolewa na baadaye notisi ya maombi hayo itachapishwa angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa sana nchini Tanzania, moja la Kingereza na lingine la Kiswahili kwa madhumuni ya kupata maoni na

mawasilisho juu ya mombi.

(2) Umma utakaribishwa kuwasilisha maoni na mawasilisho ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapishwa kwa notisi, na maoni na mawasilisho yaliyotolewa yatazingatiwa na Mamlaka katika kufikia uamuzi juu ya maombi husika.

Utoaji wa leseni

7.-(1) Mamlaka baada ya kumalizika kwa siku ishirini na moja itafanya tathmini ya maombi ya leseni na kuamua iwapo-

(a) ikubali maombi na kutoa leseni;
(b) irudishe maombi;
(c) ikatae maombi; au
(d) itoe msamaha .

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), leseni ya usafirishaji umeme itatolewa kwa taasisi ya usafirishaji umeme inayomilikiwa na Serikali.

(3) Mamlaka wakati wa kufanya uamuzi iwapo itoe, ikatae au itoe msamaha katika maombi ya leseni itazingatia yafuatayo:

(a) utunzaji wa mazingira;
(b) umuhimu na manufaa ya kiuchumi ya mradi kwa muombaji na umma kwa ujumla;
(c) maoni na mawasilisho yaliyopokelewa kutoka kwa umma, kama yapo;
(d) miundombinu ya mtu anayepewa leseni inakidhi matakwa yafuatayo:
    (i) usalama;
    (ii) afya;
    (iii) ulinzi;
    (iv) usalama dhidi ya vitu hatarishi;
    (v) utunzaji wa mazingira;
    (vi) matakwa ya mipango miji na vijiji; na
(e) suala lolote mahsusi linalohusiana na utoaji bora wa huduma za biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi, uzalishaji, usambazaji na huduma za usafirishaji ndani ya Tanzania.

(4) Endapo leseni iliyotolewa chini ya kanuni hii itakwisha muda wake, mmiliki wa leseni anaweza kuomba kuhuisha au kuongeza muda wa leseni kwa utaratibu utakaoainishwa na Mamlaka.

(5) Maombi ya kuhuisha au kuongeza muda wa leseni yataambatishwa na taarifa au nyaraka zinazohusiana na masuala ya kiudhibiti kama Mamlaka itakavyohitaji.

Maombi ya leseni ya muda

8.-(1) Mtu anayetaka kufanya shughuli inayodhibitiwa, kabla ya kuomba leseni anaweza kuomba leseni ya muda mfupi kwa Mamlaka kwa nia ya kufanya shughuli za maandalizi na shughuli nyingine muhimu kwa ajili ya kuomba leseni.

(2) Maombi ya leseni ya muda mfupi yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa muundo ulioainishwa na yataambatishwa na:

(a) nakala zilizothibitishwa za nyaraka za usajili wa mwombaji ;
(b) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;
(c) mpango wa fedha za kutekeleza mradi;
(d) vyeti vya usajili wa Utambulisho wa Mlipa Kodi na Kodi ya Ongezeko la Thamani;
(e) nakala ya cheti cha tathmini ya athari za mazingira na jamii au uthibitisho wa kuanza mchakato wa kupata cheti.

Sura ya 191

(3) Mwombaji pamoja na nyaraka zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (2), atawasilisha:

(a) kwa leseni ya uzalishaji:
 (i) ramani ya mpangilio wa matumizi ya eneo;
 (ii) teknolojia na uwezo wa uzalishaji;
 (iii) ratiba ya ujenzi;
 (iv) barua ya kuunga mkono maombi kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya umeme;
 (v) uthibitisho wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;
 (vi) uthibitisho wa haki ya kutumia maji kwa waombaji wanaotaka kuzalisha umeme kwa kutumia maji;
 (vii) uthibitisho wa haki ya kutumia ardhi kuweka miundombinu ya umeme au uthibitisho wa kuanza mchakato wa kupata haki hizo;

(viii) uthibitisho wa kibali cha kuendeleza eneo ikiwa ni pamoja na kibali cha ujenzi, kama kipo;

(ix) taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu au andiko la mradi; na

(i) mkataba wa kuuziana umeme, makubaliano au barua ya kuonesha nia, yoyote itakayotumika;

(b) kwa leseni ya usafirishaji:

(i) uthibitisho wa upatikanaji wa nishati ya umeme itakayosafirishwa ikiwemo mkataba wa mauziano ya umeme, leseni ya kununua umeme nje ya mipaka ya nchi, au mkataba wowote wa kutumia mfumo wa usafirishaji;

(ii) maelezo ya eneo la huduma;

(iii) maelezo ya mtandao wa usafirishaji;

(iv) haki ya njia au uthibitisho wa kuanza mchakato wa upatikanaji wa haki hiyo;

(v) ratiba ya ujenzi;

(vi) taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu;

(vii) mpango wa upanuzi wa mtandao wa usafirishaji, kama upo; na

(viii) ramani ya eneo la huduma linalokusudiwa.

(c) kwa leseni ya usambazaji:

(i) barua ya kuunga mkono maombi kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya umeme;

(ii) uthibitisho wa kuunga mkono mradi kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;

(iii) uthibitisho wa upatikanaji wa nishati ya umeme itakayosambazwa;

(iv) taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu;

(v) maelezo ya eneo linalokusudiwa kusambaziwa huduma;

(vi) maelezo ya mtandao wa usambazaji;

(vii) haki ya njia au uthibitisho wa kuanza kwa mchakato wa upatikanaji wa haki hiyo;

(viii) ratiba ya ujenzi; na

(ix) mpango wa upanuzi, kama upo.

Kutangazwa kwa maombi ya leseni ya muda

9.-(1) Maombi ya leseni ya muda yaliyopokelewa na Mamlaka yatafanyiwa tathmini kwa ajili ya kujiridhisha na usahihi wake na uhalali wa taarifa zilizotolewa na baada ya hapo, notisi ya maombi hayo itachapishwa angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa kwa wingi nchini Tanzania, moja la Kingereza na lingine la Kiswahili kwa madhumuni ya kupata maoni juu ya maombi hayo.

(2) Umma utakaribishwa kutoa maoni na mawasilisho ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapishwa notisi, na maoni na mawasilisho yaliyotolewa yatatumiwa na Mamlaka katika kufikia uamuzi juu ya maombi husika.

Utoaji wa leseni ya muda

10.-(1) Mamlaka baada ya ukomo wa siku ishirini na moja itafanya tathmini ya maombi ya leseni na kufanya uamuzi ikizingatia-

(a) manufaa ya kiuchumi na ufanisi wa mradi kwa muombaji na umma;

(b) maoni au mawasilisho kutoka kwa umma, kama yapo;

(2) Endapo leseni ya muda mfupi iliyotolewa chini ya kanuni hii inakwisha muda wake, mmiliki wa leseni anaweza kuomba kuhuisha au kuongeza muda wa leseni kwa utaratibu utakaoainishwa na Mamlaka..

(3) Maombi ya kuhuisha au kuongeza muda wa leseni ya muda mfupi yataambatishwa na taarifa au nyaraka zinazohusiana na masuala ya kiudhibiti kama itakavyohitajika na Mamlaka.

Msamaha

11.-(1) Mtu ambaye anafanya au anakusudia kufanya shughuli inayodhibitiwa na ana sababu za kutosha za kushindwa kukidhi matakwa ya leseni anaweza kuwasilisha maombi kwa Mamlaka ya kusamehewa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 8 cha Sheria.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote anayefanya-

(a) shughuli ya uzalishaji chini ya megawati moja; au

(b) shughuli ya usambazaji nje ya gridi katika maeneo ya vijijini ambapo mahitaji ya juu katika

mfumo ni chini ya megawati moja,

atasamehewa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 8 cha Sheria.

(3) Maombi ya msamaha chini ya kanuni ndogo ya (1) yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa maandishi yakieleza yafuatayo:

(a) maelezo ya mradi yakijumuisha wanahisa wa muombaji, maelezo ya mtambo, maelezo ya eneo na eneo la huduma linalokusudiwa; na

(b) sababu za maombi ya msamaha.

(4) Mtu aliyesamehewa kutekeleza matakwa ya kifungu cha 8 cha Sheria atajisajili kwa Mamlaka na kutoa taarifa sahihi kuhusiana na huduma za uzalishaji au usambazaji anazozitoa.

(5) Isipokuwa kama itahitajika vinginevyo na Mamlaka, shughuli yoyote ya uzalishaji chini ya megawati moja zinazokusudiwa kwa matumizi binafsi zitasamehewa matakwa ya usajili.

Kutangaz wa kwa ombi la msamaha

12.-(1) Baada ya kupokea ombi lililowasilishwa chini ya kanuni ya 11, Mamlaka itatangaza notisi ya ombi hilo angalau kwenye magazeti mawili yanayosambazwa sana kwenye eneo kubwa Tanzania, moja la Kiingereza na moja la Kiswahili, kwa lengo la kupata maoni na mawasilisho katika ombi hilo.

(2) Umma utakaribishwa kutoa maoni na mawasilisho ndani ya siku ishirini na moja kutoka tarehe ya kuchapisha notisi, na maoni na mawasililisho yaliyotolewa yatazingatiwa na Mamlaka katika kufikia uamuzi juu ya ombi husika

Utoaji wa msamaha

13.-(1) Mamlaka baada ya kuisha kwa siku ishirini na moja itaendelea kufanya tathmini ya maombi na kufanya uamuzi wa kukubali au kukataa ombi hilo kwa kuzingatia vigezo na masharti kama itakavyoona inafaa.

(2) Mamlaka wakati wa kufanya uamuzi wa kutoa leseni, kukataa au kutoa msamaha wa kutokuwa na leseni, itazingatia yafuatayo:

(a) uzito wa sababu zilizowasilishwa kuunga mkono ombi la msamaha;

(b) maslahi ya umma; na

(c) maoni na mawasilisho yaliyopokelewa kutoka

kwa umma, kama yapo.

Sababu za uamuzi

14. Mamlaka, endapo inakataa au kurejesha ombi la leseni au msamaha itamtaarifu mwombaji uamuzi huo kwa maandishindani ya siku kumi na nne ikijumuisha sababu za uamuzi huo.

Rufaa

Sura ya 285

15. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka anaweza kukata rufaa katika Baraza la Ushindani kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Ushindani.

Muda na uhamisho wa leseni

16.-(1) Muda wa leseni na leseni ya muda mfupi utaainishwa katika leseni husika.

(2) Leseni itaendelea kuwa halali kwa muda iliotolewa isipokuwa kwamba, Mamlaka inaweza kuhuisha au kuongeza muda wa leseni kwa ombi la maandishi la mtu mwenye leseni kama itakavyoona inafaa.

(3) Leseni au leseni ya muda mfupi haita hamishiwa kwa mtu mwingine bila kibali cha maandishi cha Mamlaka.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (3), endapo mtu wa tatu anakuwa mmiliki wa hisa nyingi kuhusiana na leseni au leseni ya muda ambayo imetolewa, mabadiliko ya umiliki yatawasilishwa kwa Mamlaka ndani ya siku kumi baada ya kupata vibali vya uhamisho kutoka mamlaka husika.

Usitishaji na ufutaji wa leseni

17.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha leseni kwa kipindi chakufikia miezi kumi na mbili endapo-

(a) kuna ukiukwaji wa masharti ya leseni; au
(b) kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria au Kanuni hizi; au
(c) mmiliki wa leseni ameshindwa kulipa tozo ya udhibiti kwa Mamlaka ambayo imebaki bila kulipwa kwa siku thelathini tangu siku ilipotakiwa kulipwa na Mamlaka imempa mwenye leseni notisi kwa maandishi kuwa malipo hayo yamecheleweshwa.

(2) Mamlaka inaweza kufuta leseni pale inapobaini kuwa mmiliki wa leseni ameshindwa kurekebisha au kuacha kutenda au kutotenda jambo linaloashiria ukiukwaji ndani ya

muda uliotolewa licha ya kuamriwa kufanya hivyo na Mamlaka.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza-

(a) kusamehe kusitisha leseni endapo inaridhika kuwa mmiliki wa leseni amejizuia na kitendo kilichosababisha kusimamishwa kwa leseni yake na sababu ya usitishwaji wa leseni hiyo haipo tena; na

(b) kuteua msimamizi atakayesimamia masuala ya mmiliki wa leseni kwa mujibu wa vigezo na masharti ya leseni kwa kipindi kitakachoainishwa na Mamlaka kwenye barua ya uteuzi, kwa minajili ya kusimamisha au kusitisha leseni na kwakuzingatia masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MMILIKI WA LESENI

Mmiliki wa leseni ya uzalishaji

18.-(1) Mmiliki wa leseni ya uzalishaji-

(a) atatoa huduma za uhakika za uzalishaji kwa wateja;

(b) ataendesha na kusimamia kituo cha uzalishaji;

(c) atatoza bei iliyoidhinishwa na Mamlaka kwa wateja; na

(d) atafanya kazi zote zinazohusiana na utoaji wa huduma za uzalishaji, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya kituo cha uzalishaji kwa mujibu wa taratibu nzuri katika tasnia ya umeme na mkataba wa mauziano ya umeme.

(2) Mmiliki wa leseni ya uzalishaji anaweza kutumia sehemu ya umeme uliozalishwa ili kukidhi mahitaji yake katika kituo cha uzalishaji.

Mmiliki wa leseni ya usafirishaji

19. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji-

(a) ataendesha shughuli za usafirishaji katika eneo la huduma;

(b) ataendesha na kusimamia mtandao wa usafirishaji;

(c) atatoza bei iliyoidhinishwa kwa wateja au kwa

mujibu wa sheria husika;

(d) atafanya kazi zote zinazohusiana na utoaji wa huduma za usafirishaji, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya kituo cha usafirishaji kwa mujibu wa taratibu nzuri katika tasnia ya umeme;

(e) ataruhusu matumizi ya miundombinu ya usafirishaji kwa washiriki wenye vigezo kwa misingi isiyo ya kibaguzi; na

(f) atachapisha utaratibu unaosimamia maombi ya uunganishwaji kwenye miundombinu ya usafirishaji.

Mmiliki wa leseni ya usambazaji

20. Mmiliki wa leseni ya usambazaji-

(a) ataendesha shughuli ya usambazaji katika eneo la huduma;

(b) ataendesha na kusimamia mtandao wa usambazaji;

(c) atatoza bei iliyoidhinishwa na Mamlaka kwa wateja;

(d) atafanya kazi zote zinazohusiana na utoaji wa huduma za usambazaji, ikiwa ni pamoja na uhandisi, ujenzi, ukarabati, uendeshaji na matengenezo ya kituo cha usambazaji kwa mujibu wa taratibu nzuri katika tasnia ya umeme;; na

(e) kwa kadiri inavyowezekana, atanunua umeme unaohitajika kutoka kwa mmiliki wa leseni ya uzalishaji mwenye gharama nafuu.

Mmiliki wa leseni ya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi

21.-(1) Mmiliki wa leseni ya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi-

(a) atafanya biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi kwa namna ambayo haihatarishi usalama wa gridi ya taifa;

(b) ataitaarifu Mamlaka kuhusu mabadiliko yoyote ya mikataba ya mauziano ya umeme ya mipaka ya nchi inayoathiri bei iliyoidhinishwa;

(c) atawasilisha kwa Mamlaka kila mwaka taarifa ya ukaguzi wa hesabu na utendaji; na

(d) atawasilisha kwa Mamlaka mkataba wa ununuzi wa umeme, usafirishaji wa umeme, pamoja na

tozo na bei zinazotumika kwa ajili ya kuidhinishwa.

Wajibu wa jumla wa mmiliki wa leseni

22. Mmiliki wa leseni wakati wa kutoa huduma inayodhibitiwa atazingatia kanuni na miongozo inayotolewa na Mamlaka na -

(a) atatoza bei zilizoidhinishwa na Mamlaka;
(b) atalipa ada na tozo zote zinazotakiwa;
(c) ataendesha shughuli zinazodhibitiwa bila ubaguzi na upendeleo wowote kwa wateja;
(d) atatoa taarifa kwa Mamlaka kabla ya kuacha kufanya shughuli inayodhibitiwa; na
(e) ataitaarifu Mamlaka kuhusu ajali zinazotokea wakati wa uendeshaji wa shughuli zake zenye leseni ndani ya muda wa masaa ishirini na nne kwa ajali zinazohusisha vifo, na kwa mwaka kwa ajali zisizohusisha vifo.

Mkataba wa huduma kwa mteja

23. Mmiliki wa leseni ya usambazaji ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya kupewa au kuhamishwa kwa leseni ataandaa na kuwasilisha mkataba wa huduma kwa wateja kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa ambao utajumuisha-

(a) ofa ya kuunganisha au kutoa huduma kwa mteja mtarajiwa baada ya kupokea ombi kutoka kwa mteja huyo;
(b) ofa ya kumuunganishia mmiliki yeyote wa leseni ya uzalishaji, ikijumuisha miradi midogo, kwa mujibu wa utaratibu ulioidhinishwa na Mamlaka;
(c) wajibu wa mmiliki wa leseni na ule wa watumiaji na suluhisho la ukiukwaji wa wajibu huo; na
(d) kiwango cha chini cha ubora wa huduma na viwango kulingana na matendo bora wa utoaji huduma katika tasnia ya umeme.

Fidia kwa hasara iliyopatika na

24.-(1) Mmiliki wa leseni atawajibika kumlipa fidia mtu yeyote ambaye ameumia au kupoteza mali zake kutokana na huduma inayodhibitiwa.

(2) Mtu ambaye ameumia au kupoteza mali zake kutokana na huduma inayodhibitiwa atawasilisha malalamiko yake kwa mmiliki wa leseni kwa lengo ya kufikia muafaka.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), endapo

Sura ya 414

muafaka hautafikiwa, mtu aliyeumia au kupoteza mali anaweza kulipeleka suala hilo kwa Mamlaka kwa ajili ya uamuzi na Mamlaka itashughulikia suala hilo kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, neno "mtu" linajumuisha msimamizi wa mali za mtu aliyefariki.

Taarifa za mwaka

25.-(1) Mmiliki wa leseni atawasilisha kwa Mamlaka taarifa ya mwaka sio zaidi ya siku thelathini baada ya kutoa hesabu zilizokaguliwa.

(2) Taarifa ya mwaka iliyoandaliwa na mmiliki wa leseni na kuwasilishwa kwa Mamlaka itatoa maelezo ya utendaji wa kiufundi na kiuchumi wa shughuli zinazodhibitiwa zilizofanyika katika mwaka husika.

Taarifa ya utendaji

26. Mmiliki wa leseni kila mwezi au wakati wowote mwingine kama Mamlaka itakavyohitaji-

(a) atatoa taarifa ya utendaji kazi wa shughuli zake zote zinazodhibitiwa kwa namna itakavyoainishwa na Mamlaka; na
(b) atawasilisha taarifa kwa Mamlaka ndani ya siku saba za mwezi unaofuata.

Ukaguzi wa kutii maagizo

27.-(1) Mamlaka kila mwaka itafanya ukaguzi wa mmiliki wa leseni kwa ajili ya kuangalia kama anatekeleza-

(a) Kanuni hizi;
(b) mkataba wa mauziano ya umeme;
(c) mkataba wowote muhimu katika uendeshaji wa shughuli za uzalishaji, usafirishaji au usambazaji; na
(d) kanuni zozote zinazohusika.

(2) Mamlaka kama itaona ni muhimu inaweza kumuajiri mkaguzi huru kufanya ukaguzi ulioelezwa kwenye kanuni ndogo ya (1) kwa niaba yake.

Mpango wa kuboresha utendaji

28. Mmiliki wa leseni ambaye utendaji wake upo chini ya viwango vinavyohitajika atawasilisha kwa Mamlaka kila mwaka mpango wa kuboresha utendaji ukijumuisha vigezo muhimu vya utendaji kulingana na-

(a) vigezo bora vya kimataifa;

(b) matendo bora ya utoaji huduma; na
(c) maelekezo yanayotolewa na Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA KIFEDHA

Utoaji taarifa za kifedha

29.-(1) Mmiliki wa leseni, ndani ya siku tisini baada ya kuanza kwa mwaka wake wa fedha, atawasilisha kwa Mamlaka bajeti yake inayohusiana na shughuli zinazodhibitiwa, ambayo itajumuisha-

(a) fedha za uendeshaji; na
(b) gharama za uwekezaji na gharama za uendeshaji.

(2) Mmiliki wa leseni, kila mwaka, atawasilisha kwa Mamlaka-

(a) ripoti za kiudhibiti za fedha ndani ya siku tisini kuanzia mwisho wa mwaka wa fedha; na
(b) taarifa za fedha zilizokaguliwa ndani ya siku thelathini baada ya kuzipokea.

Viwango vya utoaji wa taarifa za kiudhibiti wa kifedha

30.-(1) Mmiliki wa leseni atawasilisha taarifa za kiudhibiti wa kifedha kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa na Mamlaka.

(2) Viwango vya utoaji wa taarifa za kiudhibiti wa kifedha na utoaji wa taarifa hizo mara kwa mara utakuwa kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Utoaji wa Taarifa za Kiudhibiti wa kifedha uliotolewa na Mamlaka.

Utunzaji wa akaunti tofauti

31.-(1) Mmiliki wa leseni atatunza akaunti tofauti kwa shughuli zisizohusiana na shughuli inayodhibitiwa.

(2) Mmiliki wa leseni mwenye leseni zaidi ya moja atatunza vitabu tofauti vya akaunti na kuwasilisha taarifa tofauti kwa kila leseni.

(3) Masharti ya kanuni ndogo ya (2) hayatahusika kwa mmiliki wa leseni ambaye anafanya shughuli zote mwenyewe ndani ya kampuni mpaka hapo soko la umeme litakapofanyiwa maboresho kulingana na kifungu cha 41 cha Sheria.

Zuio la mwingilia

32. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa fedha za shughuli inayodhibitiwa hazigharamii -

no wa ruzuku

(a) shughuli nyingine yenye leseni inayodhibitiwa; au

(b) shughuli nyingine yenye leseni inayodhibitiwa na shughuli nyingine yoyote ikijumuisha shughuli za washirika wake.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA KIUFUNDI

### *Sehemu Ndogo ya Kwanza*
### *Shughuli za Uzalishaji*

Mpango wa usitishaji wa huduma na matengenezo

33. Mmiliki wa leseni ya kuzalisha-

(a) atafanya matengenezo ya kinga ya mtambo kama ilivyopangwa kwa mujibu wa maelezo ya watengenezaji ili kuhakikisha muendelezo na uhakika wa huduma za uzalishaji; na

(b) atatoa taarifa ya maandishi kwa Mamlaka kuhusu vipindi vilivyopangwa vya kusitisha huduma kwa muda kwa ajili ya matengenezo kwa kipindi kisichopungua siku tisini kabla ya kusitishwa kwa huduma.

Kukatiza huduma na matengezezo ya dharura

34. Mmiliki wa leseni ya kuzalisha-

(a) atachukua hatua stahiki kurejesha huduma za uzalishaji pale ambapo usambazaji na usafirishaji wa umeme kwa mteja katika kituo cha kuunganisha umepunguzwa au kukatizwa kwa sababu yoyote isipokuwa kusitishwa kusikopangwa;

(b) mara baada ya kufahamishwa kuhusu uharibifu wowote wa mtambo au kifaa unaoleta hatari au athari ya kujeruhi umma au mali, ataondoa hatari au athari hiyo kabla ya kufanya ukarabati au matengenezo yoyote ya dharura; na

(c) atakarabati mara moja mtambo au vifaa vilivyoharibika ikiwemo hitilafu nyingine kwenye kituo cha uzalishaji na kufanya mtambo au kifaa hicho kuanza kazi.

Taarifa ya

35. Mmiliki wa leseni ya uzalishaji-

kukatizwa kwa huduma

(a) ndani ya siku saba kabla ya usitishaji wa huduma uliopangwa, ataitaarifu Mamlaka na wateja kwa maandishi kwamba huduma ya uzalishaji itakatizwa kwa madhumuni ya kufanya ukarabati, matengenezo ya kiusalama au sababu nyingine yoyote iliyo nje ya uwezo wa mmiliki wa leseni ya uzalishaji; na

(b) ndani ya masaa ishirini na nne, atawataarifu wateja na kutoa taarifa ya maandishi kwa Mamlaka kwamba huduma ya uzalishaji imekatizwa kwa madhumuni ya kufanya matengenezo ya dharura au kwa sababu nyingine yoyote iliyo nje ya uwezo wa mmiliki wa leseni, pale ambapo kukatizwa huko kumeathiri utoaji wa huduma za uzalishaji kwa zaidi ya saa ishirini na nne.

Uhakika wa upatikanaji wa umeme

36. Mmiliki wa leseni ya uzalishaji atahakikisha kwamba, kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa leseni, na wakati wote hadi mwisho wa ukomo wa leseni, anakuwa na uhakika wa nyenzo zinazohitajika kwa shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na vipuri, mafuta na maji kwa ubora na kiwango cha kutosha kukidhi mahitaji ya umeme.

Upimaji wa umeme

37. Mmiliki wa leseni ya uzalishaji-

(a) atafunga mita za kupima umeme na nyenzo nyingine zinazohitajika kwa ajili ya kupima umeme, kwa mujibu wa kanuni na taratibu za vipimo na viwango vilivyoainishwa katika makubaliano yaliyoingiwa kati ya mmiliki wa leseni na mtu mwingine yeyote;

(b) atahakikisha mita za umeme zina usahihi kwa kiwango cha ukomo kinachokubalika na kisichozidi asilimia sifuri nukta tano (0.5%);

(c) atathibitisha usahihi wa mita na kuhakikisha kwamba mita zote zinatoa usomaji sahihi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo katika mkataba wa ununuzi wa umeme;

(d) atachukua hatua stahiki kuzuia kuchezewa na kuharibiwa kwa mita; na

(e) atapima, kutunza na kubadilisha mita kulingana

na mapendekezo ya watengenezaji.

Majaribio na uhakiki

38.-(1) Mmiliki wa leseni ya uzalishaji atafanya majaribio ya-

(a) uwezo wa kutegemewa wa kituo cha kuzalisha umeme na uhakiki kulingana na vigezo na masharti ya mkataba wa manunuzi ya umeme; na

(b) kituo cha uzalishaji endapo kutakuwa na ongezeko la uwezo au kuboreshwa kwa kituo.

(2) Mmiliki wa leseni ya uzalishaji, ndani ya siku thelathini za kazi baada ya kufanya majaribio kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), atawasilisha taarifa ya majaribio hayo kwa Mamlaka.

(3) Mmiliki wa leseni ya uzalishaji ataruhusu Mamlaka kushuhudia upimaji unaofanyika chini ya kanuni ndogo ya (1).

*Sehemu Ndogo ya Pili*

*Wajibu wa kiufundi wa mmiliki wa leseni ya usafirishaji umeme*

Ruhusa na ofa ya kujiunga au kutoa huduma ya usafirishaji umeme

39. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji wa umeme-

(a) atatoa ruhusa ya kutumia mtandao wa usafirishaji wa umeme kwa washiriki wote wenye vigezo kwa misingi ya haki, inayofaa na isiyokuwa ya kibaguzi;

(b) atatoa huduma za usafirishaji zinazohitajika ili kuruhusu kuunganishwa, kukatwa na kuunganishwa tena kwa au kutoka kwenye mtandao wake wa usafirishaji kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa uunganishaji wa mfumo wa usafirishaji unaohusika, kanuni na viwango vilivyotolewa na Mamlaka;

(c) ataruhusu kuunganishwa kwenye mtandao wake wa usafirishaji kwa masharti ya haki, yanayofaa na yasiyo ya kibaguzi kwa mtu yeyote aliyeingia mkataba wa kuunganishwa kwenye mfumo wa usafirishaji wa umeme au mkataba wa matumizi ya mfumo wa usafirishaji wa nishati;

(d) baada ya kupokea maombi ya kuunganishwa kwenye mtandao wa usafirishaji, atatathmini maombi hayo kwa mujibu wa kanuni, miongozo,

amri na maelekezo ya Mamlaka;

(e) atachukulia mkataba wa kuunganishwa katika mtandao wa usafirishaji na mkataba wa kutumia mtandao wa usafirishaji kuwa ni mikataba tofauti inayotofautiana na mkataba mwingine wowote wa mauzo ya umeme;

(f) atatoa mkataba wa kuunganishwa katika mtandao wa usafirishaji na mpango wa utekelezaji wa unganisho halisi kwa mshiriki yeyote katika soko aliye ndani ya eneo la huduma ambaye anataka kuunganishwa katika mtandao wa usafirishaji katika kipindi kisichozidi siku sitini za kazi baada ya kupokea ombi la maandishi la kuunganishwa,;

(g) atatoa fursa kwa mteja yeyote kuunganishwa kwenye mtandao wa usafirishaji endapo kuna uwezo wa kutosha katika mtandao wa usafirishaji bila kuathiri aya ya (f),;

(h) katika kipindi kisichozidi siku thelathini za kazi baada ya kujulishwa juu ya kukubaliwa kwa ofa iliyotolewa katika aya ya (f)-

(i) atakamilisha mkataba wa matumizi ya mtandao wa usafirishaji wa umeme na mtu huyo; na

(ii) atamuunganisha mtu huyo;

(i) bila kuathiri masharti ya aya ya (f), (g) na (h) na baada ya kupokea ombi la maandishi, atatoa ofa ya kutoa huduma zinazoombwa ndani ya muda mwafaka kwa kuzingatia ugumu wa huduma zinazoombwa na taratibu zinazokubalika; na

(j) atatekeleza huduma zote zinazohitajika ili kuruhusu kuunganishwa, kukatwa na kuunganishwa tena kwa au kutoka kwa mtandao wa usafirishaji.

Wajibu wa jumla wa mmiliki wa leseni ya usafirishaji wa umeme

40. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji-

(a) atasimamia, kutunza na kuendesha mtandao wa usafirishaji ili kuhakikisha kuwa katika hali ya kawaida umeme unaendelea kuhamishwa katika kituo cha kusafirishwa kwa mujibu wa-

(i) miundo ya kiufundi inayotumika; na

(ii) viwango vya uhakika na ubora wa huduma

vilivyoidhinishwa na Mamlaka;

(b) atapunguza idadi ya kukatizwa au kupungua kwa uwezo uliokadiriwa katika kituo cha kuunganisha umeme kwa mujibu wa Matendo Bora ya Utoaji Huduma; na

(c) atarejesha umeme stahiki haraka iwezekanavyo kufuatia kukatizwa aidha-

(i) kwenye kituo cha kuunganisha katika mtandao wa usafirishaji wa umeme; au

(ii) kwenye mtandao wa usafirishaji wa umeme.

Haki za mmiliki wa leseni ya usafirishaji

41. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atakuwa na haki ya-

(a) kuondoa kifaa chochote cha mtumiaji wa mfumo wa usafirishaji ambacho kinaathiri vibaya uadilifu na usalama wa mtandao wa usafirishaji;

(b) kutumia mfumo na huduma za muendeshaji wa mfumo na muendesha soko kwa misingi isiyo ya kibaguzi;

(c) kufanya kazi na waendeshaji wa mfumo na soko kwa lengo la-

(i) kuratibu ukatikaji wa umeme;

(ii) kuwasilisha ubora na uwezo wa mitambo yake; na

(iii) kuamua juu ya athari zinazohusiana na ukataji umeme kwa mitambo yake;

(d) kupata taarifa, taarifa zisizo za siri na kuingia kwenye tovuti ya mwendeshaji wa mfumo na soko; na

(e) endapo mwendeshaji wa mfumo na soko au mtumiaji wa usafirishaji wa umeme anashindwa kuzingatia kanuni, kuwasilisha lalamiko kwa-

(i) mwendeshaji wa mfumo na soko; au

(ii) Mamlaka.

Taarifa ya utendaji wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme

42. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atatoa kwa Mamlaka, taarifa ya kina ya shughuli zake za mtandao wa usafirishaji wa umeme, ikijumuisha uwezo, ukataji, hasara, ufanisi na uhakika kadri Mamlaka itakavyohitaji.

Mpango wa mtandao wa usafirishaji na utwaaji wa ardhi

43.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji ataandaa mpango wa uendelezaji wa mtandao wa usafirishaji.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, atawasilisha mpango ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa Mamlaka kwa lengo la kuidhinishwa ndani ya siku sitini kabla ya kuanza kwa mwaka.

(3) Mpango ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) utatekelezwa kwa mujibu wa mipango mahsusi ilioyoandaliwa kwa lengo la kuboresha mtandao wa usafirishaji wa umeme katika kiwango kinachokubalika cha kiufundi na kiuchumi, kwa kuzingatia-

(a) viwango vya afya, usalama na mazingira;
(b) ongezeko la mahitaji ya umeme, na
(c) upatikanaji na uhakika wa huduma za usafirishaji kwa wateja.

(4) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji ataomba kwa Mamlaka husika haki ya njia ya kupitisha miundombinu kwenye kipande chochote cha ardhi ili kuwezesha kufikia, kujenga, kutunza au kupanua mtandao wa usafirishaji.

(5) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atachukua hatua stahiki mara kwa mara ili kulinda maslahi yake chini ya kanuni ndogo ya (4).

Mpango wa upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji

44.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atawasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya mapitio, mpango wa upanuzi wa mtandao wa usafirishaji ambao utakuwa na uthibitisho wa upanuzi au uendelezaji wa mtandao wa usafirishaji.

(2) Mpango wa upanuzi wa mtandao wa usafirishaji-

(a) utazingatia sera ya kitaifa ya nishati;
(b) utakuwa unaowezekana kiufundi, kimazingira na kiuchumi;
(c) utazingatia-
   (i) mahitaji ya matumizi ya umeme yaliyotolewa na mwendesha mfumo na soko;
   (ii) mahitaji ya viunganishi au upanuzi uliokubaliwa wa viunganishi vilivyopo;
   (iii) viwango vilivyoidhinishwa vya uhakika na ubora wa huduma;
   (iv) Mpango wa Muda Mrefu wa Kuendeleza Umeme; na

(v) maombi yoyote ya upanuzi yaliyowasilishwa na watumiaji wa mtandao wa usafirishaji au waombaji wapya wanaotaka kutumia mtandao wa usafirishaji.

Uwiano wa nguvu za umeme

45. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, ili kuhakikisha kwamba mtandao wa usafirishaji unakuwa na uwiano sahihi wa nguvu za umeme-

(a) atafunga vifaa vinavyoendana na Matendo Bora ya Utoaji Huduma katika tasnia ya umeme; na

(b) atahakikisha kuwa mikataba yote ya ugavi wa umeme iliyoingiwa na mmiliki wa leseni inafafanua wajibu wa upande wa pili wa kufunga vifaa vya uboreshaji wa uwiano wa nguvu za umeme kwenye kituo cha kupokelea umeme.

Upotevu katika usafirishaji

46.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atapunguza aina yoyote ya upotevu wa umeme katika mtandao wa usafirishaji hadi kiwango kilichoidhinishwa na Mamlaka.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atawasilisha kwa Mamlaka ndani ya siku thelathini za-

(a) mwaka unaofuata, taarifa ya upotevu wa umeme kwenye mtandao wake katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, pamoja na mpangowa kupunguza upotevu huo; na

(b) za robo mwaka unaofuata, taarifa ya robo mwaka ya upotevu wa umeme, pamoja na mipango kupunguza upotevu huo.

(3) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atatekeleza malengo yoyote yaliyotolewa na Mamlaka kuhusiana na upunguzaji wa upotevu wa umeme.

kuzingatia maelekezo kutoka kwa mwendeshaji wa mfumo na soko

47. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atafuata maelekezo ya mwendeshaji wa mfumo na mwendeshaji wa soko wakati wote.

Kuwasilisha taarifa

48.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atatoa taarifa zote zinazohusiana na mtandao wa usambazaji endapo

kwa mwendeshaji wa mfumo na soko

atapokea ombi la maandishi kutoka kwa mwendeshaji wa mfumo na soko.

(2) Taarifa iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) inaweza kuwa nyongeza kwa taarifa yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni za soko au leseni.

(3) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji hatanunua au kuuza umeme, isipokuwa-

(a) kwa lengo la kufidia hasara kwenye mtandao wa usafirishaji ikijumuisha uendeshaji wa vituo vya mashine umba; au

(b) kama mteja wa mifumo mingine, kukidhi mahitaji yake ya kiutawala.

(4) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, endapo kifaa cha mtumiaji wa mfumo wa usafirishaji kitashindwa kukidhi matakwa na viwango vya kiufundi vilivyowekwa, atabaini na kutoa taarifa kuhusu kushindwa huko kwa-

(a) Mamlaka; na

(b) mwendeshaji wa mfumo na soko.

(5) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji-

(a) atapokea, kujibu na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na mwendeshaji wa mfumo na soko, isipokuwa kama kufanya hivyo kutaathiri vifaa au wafanyakazi wa mmiliki wa leseni;

(b) atamtaarifu mwendeshaji wa mfumo na soko kuhusu-

(i) mabadiliko yoyote katika miundombinu ya usafirishaji; au

(ii) changamoto inayomkabili mmiliki wa leseni kuhusiana na mpango wa upanuzi wa mfumo wa usafirishaji au uratibu wa mfumo wa usafirishaji;

(c) atawasilisha kwa mwendeshaji wa mfumo na soko taarifa zinazotakiwa chini ya-

(i) Sheria;

(ii) Kanuni hizi;

(iii) leseni; na

(iv) kanuni za soko;

(d) endapo kutatokea mabadiliko yoyote katika taarifa iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya 5(c), atamtaarifu mwendeshaji wa mfumo na soko ndani ya siku saba za kazi tangu tarehe ya

mabadiliko hayo.

Maandalizi kukabiliana na dharura

49.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atachukua hatua stahiki kama itakavyotakiwa ili -
(a) kujiandaa na dharura;
(b) kurekebisha mtandao wa usafilishaji baada ya janga; na
(c) kushiriki katika majaribio.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji ataweka utaratibu kuhakikisha uendeshaji salama na endelevu wa mfumo wa umeme wakati wa hali za dharura, kwa kuzingatia kanuni za soko na kanuni na viwango vingine vyovyote husika vilivyowekwa au kuidhinishwa na Mamlaka.

Matengenezo ya kawaida

50.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji-
(a) atafanya matengenezo ya kawaida kuhakikisha uendelevu na uhakika wa huduma za usafirishaji;
(b) atafanya matengenezo ya kawaida kwenye mtandao wa usafirihsaji kwa mujibu wa kanuni, maelekezo na ratiba iliyoidhinishwa na Mamlaka;
(c) atafanya matengenezo ya dharura au makubwa kwenye vifaa vya mtandao wa usafirishaji ili kuhakikisha uendelevu na uhakika wa usafirishaji wa umeme; na
(d) kwa kuzingatia mipango ya matengenezo na uwekezaji ulioidhinishwa na Mamlaka, atabadilisha na kukarabati vifaa vya mtandao ambavyo-
   (i) vimekaribia mwisho wa matumizi; au
   (ii) vimechakaa kwa sababu yoyote.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atapanga na kuratibu shughuli za matengenezo ya kila mwaka na ya muda mrefu kwa kushirikiana na mwendeshaji wa mfumo na soko.

(3) Mipango na ratiba ya matengenezo iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2) itazingatia-
(a) kanuni na miongozo inayotolewa na Mamlaka; na
(b) kupunguza gharama ya jumla ya upelekaji wa umeme huku ikidumisha uhakika wa mtandao wa usafirishaji.

Matengene

51. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji-

zo ya dharura na ukarabati

(a) pale ambapo kifaa au mtambo umeharibika na kina uwezo kusababisha hatari au athari ya kujeruhi umma au mali, mara baada ya kufahamishwa kuhusu uharibifu huo, ataondoa hatari au athari hiyo kabla ya kufanya matengenezo au ukarabati wowote wa dharura;
(b) atakarabati haraka sehemu zilizoharibika za mtandao wa usafirishaji na kuwaunganisha haraka iwezekanavyo; na
(c) atafanya shughuli zote za ubadilishaji na ukarabati zinazohitajika kwa mujibu wa mipango ya ukarabati na uwekezaji iliyoidhinishwa na Mamlaka.

Matengenezo kinga

52. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atahakikisha kuwa katizo la huduma ya usafirishaji uliopangwa linakuwa la muda mfupi kadri iwezekanavyo.

Katizo la huduma lililopangwa

53. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji ataitaarifu Mamlaka kwa maandishi endapo kutatokea kukatizwa kwa huduma kwa ajili ya ukarabati au matengenezo ya kiusalama ya dharura ambayo yanaathiri huduma za usafirishaji kwa zaidi ya siku mbili mfululizo.

katizo la umeme lisilopangwa

54. Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, kwa kushauriana na mwendeshaji wa mfumo na soko, atarejesha huduma baada ya katizo kwa muda mfupi kadri iwezekanavyo.

Notisi ya katizo la huduma

55.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, wakati anakusudia kufanya matengenezo ya kiusalama, mabadiliko, urekebishaji au ujenzi mwingine wowote ambao unaweza kusababisha kukatizwa au kupunguzwa kwa huduma za usafirishaji, atatoa notisi kwa umma, kwa kipindi kisichopungua siku tatu za kazi kabla ya kuanza shughuli hizo.

(2) Notisi iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha tarehe na saa ya-
(a) kukatizwa kwa huduma ya usafirishaji; na
(b) marejesho yaliyokusudiwa.

Mita

56.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atafunga, kutunza, na kuthibitisha usahihi wa meta zilizofungwa katika vituo vyote vya kuchukulia umeme kwenye mtandao wa usafirishaji.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, kwa kila meta iliyofungwa chini ya kanuni ndogo ya (1), atazingatia viwango vya upimaji na kanuni zilizotungwa na Mamlaka.

(3) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atawasilisha kwa washiriki wa soko data zote zinazohitajika ili kukokotoa mafanikio ya mikataba ya pande mbili, au kutatua mgogoro wowote unaohusiana na mikataba ya pande mbili.

(4) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji atakadiria umeme uliotumika katika kipindi ambacho mita imesimama au ina hitilafu za kiutendaji kwa mujibu wa kanuni za soko.

Mpango wa kuboresha utendaji

57.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kupokea leseni, atathibitisha msingi wa uendeshaji na usimamizi ambao utatumika kuweka mpango wa kuboresha utendaji utakaoidhinishwa na Mamlaka.

(2) Mpango unaotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (1)-

(a) utajumuisha malengo mahsusi ya kuboresha huduma kwa kutengeneza viashiria muhimu vya utendaji na kuanzisha mbinu za kufuatilia mafanikio; na

(b) pale inapolazimu, utaendelezwa kwa mujibu wa kanuni au maelekezo ya Mamlaka.

(3) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, katika kila mwaka, atapitia na kuwasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa mpango ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1).

Mpango wa kuhakiki ubora

58.-(1) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji ataanda mpango wa kufikia kiwango cha juu cha ubora kuhusu huduma za usafirishaji na kufanya marekebisho stahiki kwa kufuata maelekezo ya Mamlaka.

(2) Mmiliki wa leseni ya usafirishaji, katika kipindi kisichozidi siku tisini baada ya kupokea leseni, atawasilisha mpango wa kuthibitisha ubora wa huduma kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa.

## *Sehemu Ndogo ya Tatu*
## *Wajibu wa kiufundi wa mmiliki wa leseni ya usambazaji*

Ruhusa na ofa ya kujiunga au kutoa huduma ya usambazaji

59. Mmiliki wa leseni ya usambazaji-
(a) atatoa huduma za usambazaji kwa watumiaji wote kwa misingi ya haki, yenye kufaa na isiyo na ubaguzi;
(b) atatekeleza shughuli zote zinazohitajika ili kuruhusu kuunganishwa, kukatwa, na kuunganishwa tena kwa au kutoka kwa mtandao wa usambazaji kwa mujibu wa kanuni za usambazaji, na kanuni zozote husika zinazotolewa au kuidhinishwa na Mamlaka; na
(c) hatapunguza au kusitisha huduma za usambazaji kwa mteja isipokuwa kama mteja huyo ameshindwa kulipa tozo au malipo ndani ya muda uliowekwa au kuzingatia vigezo na masharti ya mkataba wa ugavi.

Mkataba wa ugavi

60.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji ataingia katika mkataba wa ugavi na kila mteja.

(2) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atahakikisha kuwa mikataba yake ya ugavi ina angalau taarifa zifuatazo:
(a) utambulisho wa mmiliki wa leseni na anwani yake;
(b) wigo wa huduma itakayotolewa;
(c) aina ya matengenezo na usaidizi wa huduma kwa wateja unaotolewa;
(d) njia ambazo wateja wanaweza kupata taarifa kuhusu tozo;
(e) wajibu na utaratibu wa kutoa taarifa ya kukosekana kwa umeme;
(f) muda wa mkataba;
(g) masharti ya kuhuisha au kusitisha mkataba; na
(h) mipangilio yoyote ya fidia au urejeshaji fedha endapo viwango vya huduma bora vilivyokubaliwa katika mkataba havitafikiwa.

Mpango wa miundombinu ya

61.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atapaswa, kwa mujibu wa kanuni zilizotolewa na Mamlaka, kutayarisha mpango wa upanuzi na uendelezaji wa mtandao wake wa

usambazaji na utwaaji wa ardhi

usambazaji.

(2) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, katika kipindi kisichopungua miezi miwili kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa kalenda, atawasilisha mpango ulioelezwa katika kanuni ndogo ya (1) kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Mpango ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) utatekelezwa kwa mujibu wa mipango mahsusi ya utekelezaji iliyoandaliwa ili kuboresha mtandao wa usambazaji katika kiwango kinachokubalika kiufundi na kiuchumi, kwa kuzingatia-

(a) viwango vya kiafya, kiusalama na kimazingira;

(b) ongezeko la matumizi ya umeme; na

(c) upatikanaji na uhakika wa huduma za usambazaji kwa wateja.

(4) Mmiliki wa leseni ya usambazaji ataomba kwa mamlaka husika haki yoyote ya njia inayohitajika katika kipande chochote cha ardhi ambayo inaweza kuhitajika kwa lengo la kufikia, kujenga, kutunza au kupanua mtandao wa usambazaji.

(5) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atachukua hatua zote kama itakavyohitajika mara kwa mara ili kulinda maslahi yake katika ardhi iliyotwaliwa chini ya kanuni ndogo ya (4).

Makadirio ya matumizi

62.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atawasilisha makadirio ya matumizi ya umeme katika kila mwaka, na katika muda wowote kama itakavyohitajika na Mamlaka.

(2) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, ataandaa na kuwasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa, mahitaji ya umeme na makadirio ya matumizi ya umeme ndani ya mtandao wake wa usambazaji, kwa miaka mitatu mfululizo.

(3) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atawasilisha kwa Mamlaka-

(a) mwenendo wa matumizi halisi ya kiasi cha umeme kilichotumiwa na kila kundi la wateja; na

(b) idadi ya wateja na muhtasari wa mahitaji ya umeme kwa kila kundi la wateja.

Uhakika na usalama

63. Mmiliki wa leseni ya usambazaji atawapa wateja

wa ugavi

wake maelezo ya mawasiliano wanayoweza kutumia kumjulisha mmiliki wa leseni kuhusu suala au tukio lolote linalohusiana na upatikanaji wa huduma za usambazaji ambalo:

(a) linasababisha hatari au linahitaji kushughulikiwa haraka; au

(b) linaathiri au kuwa na uwezekano wa kuathiri usalama, upatikanaji au ubora wa huduma za usambazaji.

Ubora wa huduma

64.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, katika kipindi kisichozidi miezi sita baada ya kupokea leseni, atawasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa, viwango vya ubora wa huduma ya usambazaji na ubora wa viwango vya usambazaji.

(2) Viwango vya ubora wa huduma na ubora wa usambazaji vilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) vitazingatia matendo bora ya utoaji huduma katika tasnia ya umeme.

(3) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, katika kipindi kisichozidi siku tisini baada ya kuidhinishwa kwa viwango vya ubora chini ya kanuni ndogo ya (1), atawasilisha mpango wa jinsi ya kufikia viwango hivyo.

Uwiano wa nguvu za umeme

65. Mmiliki wa leseni ya usambazaji atafunga vifaa vinavyohitajika ili kuhakikisha kuwa uwiano wa nguvu za umeme katika mtandao wa usambazaji unafikia viwango vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na ufungaji wa vifaa vya kupima ubora katika eneo husika katika mtandao.

Upotevu wa umeme kwenye mfumo wa usambazaji

66.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji-

(a) ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, atawasilisha utafiti unaobainisha kiwango cha upotevu wa kiufundi na kibiashara katika mtandao wa usambazaji ikijumuisha uunganishaji usio halali; na

(b) atapendekeza malengo yanayoweza kufikiwa ya kupunguza upotevu kwa ajili ya kuidhinishwa na Mamlaka.

(2) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atawasilisha kwa

Mamlaka taarifa ya upotevu wa umeme kwenye mtandao wa usambazaji katika mwaka uliopita, pamoja na mpango wa kupunguza upotevu huo.

Maandalizi ya kukabiliana na dharura

67. Mmiliki wa leseni ya usambazaji-

(a) atachukua hatua ndani ya mipaka ya kiufundi inayokubalika kadiri anavyoweza kwa ajili ya maandalizi ya dharura na urejeshaji wa mtandao wa usambazaji; na

(b) ataweka na kutekeleza taratibu ndani ya mipaka ya kiufundi inayokubalika ili kuhakikisha uendeshaji salama na endelevu wa mtandao wa usambazaji katika hali za dharura.

Mpango wa usitishaji umeme kwa ajili ya matenegezo kinga

68.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atafanya matengenezo kinga ili kuhakikisha uendelevu na uhakika wa huduma za usambazaji.

(2) Mmiliki wa leseni ya usambazaji atatangaza kwa umma muda uliopangwa wa katizo la umeme kwa ajili ya matengenezo katika kipindi kisichopungua siku saba kabla ya katizo lililopangwa.

(3) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, wakati wa kufanya matengenezo kinga, kubadilisha, kurejesha au ujenzi mwingine wowote ambao unaweza kusababisha kusimamishwa kwa utoaji wa huduma za usambazaji kwa zaidi ya saa ishirini na nne-

(a) ataitaarifu Mamlaka na umma angalau siku tatu kabla ya kusimamisha utoaji wa huduma ya usambazaji; na

(b) atahakikisha kuwa katizo lolote la huduma ya usambazaji lililopangwa, limepangwa kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Katizo la huduma na matengenezo ya dharura

69. Mmiliki wa leseni ya usambazaji-

(a) atachukua hatua zinazofaa mara moja ili kurejesha huduma kwa wateja endapo kuna katizo la usambazaji lililotokana na sababu yoyote ikiwemo katizo lisilopangwa;

(b) endapo kutatokea uharibifu wowote wa mtambo au kifaa unaoleta hatari au athari kwa umma au mali na mara baada ya kufahamishwa kuhusu

uharibifu huo, ataondoa hatari au athari hiyo kabla ya kufanya matengenezo au ukarabati wowote wa dharura; na

(c) atakarabati mara moja mtambo au vifaa vilivyoharibika na kasoro nyingine katika kituo na kumuunganisha tena mteja kama ilivyoainishwa katika mkataba wa huduma kwa wateja.

Taarifa ya katizo la huduma ya usambazaji

70. Mmiliki wa leseni ya usambazaji ataitaarifu Mamlaka na wateja kwa maandishi, endapo huduma ya usambazaji itakatizwa kwa madhumuni ya kufanya-

(a) ukarabati au matengenezo kinga na katizo hilo utaathiri utoaji wa huduma za usambazaji; na

(b) matengenezo ya dharura, endapo katizo hilo limeathiri utoaji wa huduma ya usambazaji kwa zaidi ya saa arobaini na nane.

Upimaji

71.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji-

(a) kutoka katika kila kituo cha kufunga mita, atawasilisha kwa mmiliki wa leseni ya uzalishaji, mmiliki wa leseni ya usafirishaji au mtu mwingine yeyote, data zote zinazohitajika ili kupima utimilifu wa wajibu wake au kutatua mgogoro wowote unaohusiana na mkataba;

(b) atafunga, kutunza na kulingana na kwa mujibu mapendekezo ya mtengenezaji, kuhakiki usahihi wa ufungaji wa meta katika vituo vyote vya wateja kuchukulia umeme kutoka katika mtandao wa usambazaji; na

(c) endapo itatokea hitilafu katika utendaji au uharibifu wowote kwenye meta kutokana na sababu yoyote iliyo nje ya uwezo wa mteja, atarekebisha hitilafu au uharibifu huo au kubadilisha meta haraka iwezekanavyo.

(2) Nishati ya umeme inayotumiwa katika kipindi ambacho meta imesimamishwa au haifanyi kazi vizuri itakadiriwa kulingana na-

(a) kwa mteja mkubwa, mikataba husika; na

(b) kwa wateja wengine wote, na pale ambapo hakuna makadirio yoyote ya mkataba, mwenendo wa matumizi yaliyopita.

Sura ya 414

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2)(b), endapo mteja hajaridhika na kiasi cha fedha kilichokadiriwa, atapeleka suala hilo kwenye Mamlaka kwa uamuzi na Mamlaka itashughulikia suala hilo kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

Kugundua na kuzuia wizi, uharibifu na kuchezea meta

72. Mmiliki wa leseni ya usambazaji atachukua hatua zote zinazofaa ili kugundua na kuzuia-

(a) wizi wa umeme katika eneo la huduma;
(b) uharibifu au hitilafu katika mtambo wowote wa umeme, meta ya umeme katika eneo la huduma;
(c) kuchezewa kwa meta yoyote ya umeme katika eneo la huduma; na
(d) matumizi yoyote ya umeme yasiyopimwa katika eneo la huduma.

Mpango wa kuboresha utendaji

73.-(1) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kupokea leseni, atathibitisha msingi wa uendeshaji na usimamizi ambao utatumika kuweka mpango wa kuboresha utendaji utakaoidhinishwa na Mamlaka.

(2) Mpango unaotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (1)-

(a) utajumuisha malengo mahsusi ya kuboresha huduma kwa kutengeneza viashiria muhimu vya utendaji na kuanzisha mbinu za kufuatilia mafanikio; na
(b) pale inapolazimu, utaendelezwa kwa mujibu wa kanuni au maelekezo ya Mamlaka.

(3) Mmiliki wa leseni ya usambazaji, katika kila mwaka, atapitia na kuwasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa mpango ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (2).

## SEHEMU YA SITA
## UTAMBUZI WA WATEJA MAALUM

Maombi ya kuwa mteja maalum

74.-(1) Mtu yeyote mwenye vigezo vinavyohitajika na anayekusudia kutambuliwa kuwa mteja maalum ataomba kwa Mamlaka katika namna iliyoainishwa kwenye Jedwali.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1)

yataambatishwa na nyaraka zifuatazo:

(a) uthibitisho wa uwezo wa matumizi ya umeme;
(b) mkataba wa usafirishaji, kama upo; na
(c) barua ya uthibitisho kutoka kwa mwenye leseni aliyekuwa akimuuzia umeme ikionesha kuwa mwombaji hana deni lolote dhidi ya mwenye leseni huyo pale inapohitajika.

Vigezo vya kuteuliwa kuwa mteja maalum

75.-(1) Ombi la kutambuliwa kama mteja maalum litakidhi vigezo vifuatavyo:

(a) mwombaji awe anahitaji kupatiwa huduma ya umeme kwa msongo usiopungua kilovolti 33;
(b) mwombaji lazima awe na mahitaji ya juu ya megawati mbili au zaidi; na
(c) endapo mwombaji anapewa huduma ya umeme na mmiliki wa leseni ya usambazaji, ni lazima apate barua kutoka kwa mmiliki wa leseni ili kuthibitisha kwa Mamlaka kuwa hakuna wajibu ambao haujatekelezwa.

(2) Bila kujalii masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kuamua kukubali maombi ya kutambuliwa kama mteja maalum pasipo mwombaji kukidhi vigezo pale ambapo itahitajika kufanya hivyo.

Haki za mteja maalum

76. Mtu yeyote aliyetambuliwa kama mteja maalum na Mamlaka atakuwa na haki zifuatazo:

(a) kununua umeme kutoka kwa mmiliki wa leseni ya uzalishaji atakayemchagua;
(b) kuingia katika mkataba wa ununuzi wa umeme na mmiliki wa leseni ya uzalishaji bila idhini ya Mamlaka; na
(c) kujadili bei ya umeme kwa kuzingatia maelewano na muuzaji.

Nguvu ya masharti haya

77. Masharti ya Sehemu hii yatakuwa na nguvu zaidi dhidi ya kanuni nyingine zozote zilizotengenezwa na Mamlaka na endapo kutatokea kutofautiana, masharti ya Sehemu hii yatatumika.

## SEHEMU YA SABA
## UFUATILIAJI NA UTEKELEZAJI

Ukaguzi

78.-(1) Mamlaka, baada ya kutoa taarifa kwa mmiliki wa leseni, itakagua miundombinu inayodhibitiwa ikiwemo nyaraka, na mmiliki wa leseni atatoa msaada unaohitajika wakati wa ukaguzi wa shughuli zake zinazodhibitiwa.

(2) Wakati wa ukaguzi Mamlaka inaweza-

(a) kutoa nakala au kuchukua dondoo kutoka kwa kitabu chochote, akaunti za hesabu au kumbukumbu zilizowekwa na mmiliki wa leseni chini ya sheria husika;

(b) kukagua mitambo, vifaa, mita na kuchukua vipimo au kurekodi data za kiufundi ikijumuisha matumizi ya nishati, msongo, masafa na kuona utekelezaji wa mikataba ya huduma kwa wateja; na

(c) kuingia kwenye mifumo ya programu ya kompyuta ya mmiliki wa leseni kama itaonekana ni lazima.

Wajibu wa Mkaguzi wakati wa ukaguzi

79.-(1) Afisa au mwakilishi wa Mamlaka wakati wa ukaguzi atafanya yafuatayo:

(a) kujitambulisha kwa mmiliki wa leseni au mteja kwa kitambulisho kilichotolewa na Mamlaka;

(b) kumweleza mmiliki wa leseni au mteja madhumuni ya ukaguzi;

(c) kutenda kwa haki, usawa na uadilifu;

(d) kutojihusisha na aina yoyote ya ubaguzi, upendeleo au unyanyasaji;

(e) kujiepusha kushiriki katika majukumu endapo endapo itaonekana kuna mgongano wa kimaslahi;

(f) kufanya ukaguzi kwa njia ya kitaalamu kwa mujibu wa mahitaji ya Kanuni hizi, kanuni, miongozo, orodha ya ukaguzi, viwango, sheria husika na matendo bora katika utoaji wa huduma;na

(g) kutotumia nguvu au lugha ya karaha, vitisho na matusi kwa mmiliki wa leseni.

(2) Mtu ambaye hajaridhika na kitendo cha afisa au mwakilishi wa Mamlaka wakati wa ukaguzi, ndani ya kipindi

cha siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kitendo hicho, anaweza kutoa taarifa kwa maaandishi kuhusu suala hilo kwa Mamlaka.

(3) Baada ya kupokea malalamiko chini ya kanuni ndogo ya (2), Mamlaka itaendelea kufanya uamuzi kwa mujibu wa utaratibu wake wa ndani.

Vitendo vilivyokatazwa kwa mkaguzi

80. Mmiliki wa leseni-

(a) hatamzuia au kumkwamisha afisa au mwakilishi wa Mamlaka katika kutekeleza wajibu aliopewa kwa mujibu wa Kanuni hizi au Sheria;

(b) hatatumia lugha ya karaha, vitisho au matusi;

(c) hatakataa au kushindwa kutii amri, maelekezo au notisi halali; na

(d) anapotakiwa kujibu swali, hatakataa au kushindwa kujibu swali hilo kwa kadri ya ufahamu, taarifa na imani yake.

## SEHEMU YA NANE
## USIMAMIZI WA CHUMBA CHA UDHIBITI

Mahitaji ya jumla

81. Mmiliki wa leseni, wakati wote wa kuendesha chumba cha udhibiti mitambo, atazingatia mahitaji yafuatayo:

(a) kuwa na angalau mwendeshaji mmoja wa chumba cha udhibiti katika kila chumba cha udhibiti;

(b) kuwa na utaratibu ulioandikwa wa kuwaongoza waendeshaji wa vyumba vya udhibiti;

(c) kuwa na utaratibu wa uendeshaji uliounganishwa na mipango ya kushughulikia dharura;

(d) muundo wa chumba cha kudhibiti kuwa na uwezo wa kuhimili majanga au matukio ya hatari yanayoweza kujitokeza;

(e) mpangilio wa chumba cha udhibiti, mpangilio wa paneli na sehemu ya kuonesha upo katika namna itakayohakikisha uendeshaji mzuri wa mtambo katika hali ya kawaida na ya dharura; na

(f) chumba cha udhibiti mitambo kinafanya kazi wakati wote.

Wajibu

82. Mmiliki wa leseni, kila wakati-

(a) ataweka na kuwa na utaratibu ulioandikwa wa usimamizi wa chumba cha udhibiti mitambo unaozingatia Kanuni hizi;

(b) atakuwa na chumba cha udhibiti kilichotengenezwa kwa kuhakikisha kwamba hatari kwa watumiaji wa chumba cha udhibiti ziko ndani ya kiwango kinachokubalika;

(c) atakuwa na chumba cha udhibiti ambacho kinakidhi madhumuni ya kudhibiti miundombinu ya umeme;

(d) atakuwa na chumba cha udhibiti ambacho kina mpango wa dharura wa kufuata wakati wa kushughulikia vitendo vya dharura visivyotegemewa kutokea, ndani ya miundombinu ya umeme;

(e) ataajiri wafanyakazi wenye ujuzi na maarifa ya kuendesha chumba cha udhibiti;

(f) atatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa waendeshaji wa vyumba vya udhibiti ili kuwawezesha kutekeleza majukumu na wajibu ulioainishwa na mmiliki wa leseni; na

(g) atatengeneza na kutunza mwongozo wa uendeshaji na matengenezo.

Utaratibu

83.-(1) Kila mmiliki wa leseni atatayarisha na kufuata mwongozo wa utaratibu ulioandikwa wa uendeshaji shughuli za kawaida, matengenezo na shughuli za dharura.

(2) Mwongozo utaeleza masuala yafuatayo:

(a) utaratibu wa usalama unaopaswa kufuatwa wakati wa matengenezo na shughuli za kawaida; na

(b) utaratibu wa kushughulikia shughuli zisizo za kawaida.

(3) Mwongozo utapitiwa na kuhuishwa na mmiliki wa leseni angalau mara moja kila mwaka.

(4) Nakala halisi ya mwongozo itatunzwa na mhusika.

(5) Nakala ya mwongozo itatunzwa mahali ambapo shughuli za uendeshaji na matengenezo zinafanyika.

Kuzingatia utaratibu

84.-(1) Mmiliki wa leseni atafahamu utaratibu wa

wa dharura

dharura na wakati wote atazingatia mpango wa maandalizi ya dharura ulioidhinishwa.

(2) Mmiliki wa leseni atajumuisha mafunzo aliyojifunza, ikiwa ni pamoja na mapitio mahsusi ya matukio au ajali zote zinazoripotiwa, katika utaratibu wake wa usimamizi wa chumba cha udhibiti na atahifadhi nyaraka za kuthibitisha kwamba kutokufuatwa kwa utaratibu kulikuwa muhimu kwa uendeshaji salama wa kituo.

(3) Mmiliki wa leseni atahakikisha kwamba mabadiliko katika kituo yanaratibiwa kati ya wawakilishi wa chumba cha udhibiti, wataalamu wa shughuli za usimamizi na wale waliopo eneo la mtambo na kwamba wataalamu waliopo eneo la mtambo wanawasiliana na wataalamu wa chumba cha udhibiti wakati wa hali ya dharura.

(4) Mmiliki wa leseni-

(a) atatoa mafunzo kwa wataalamu wa uendeshaji husika ili kuhakikisha kwamba wana ujuzi wa taratibu za dharura; na

(b) atakagua shughuli za wafanyakazi ili kubaini kama utaratibu ulifuatwa ipasavyo katika kila hali ya dharura.

(5) Mmiliki wa leseni ataanzisha na kutunza mawasiliano na zimamoto, polisi na maafisa wengine wa umma ili-

(a) kuelewa wajibu na rasilimali za kila chombo husika cha kukabiliana na dharura;

(b) kufahamu chombo husika cha kukabiliana na dharura na uwezo wake katika kukabiliana na hali ya dharura;

(c) kutambua aina za dharura ambazo atazitolea taarifa kwa shirika husika la kukabiliana na dharura; na

(d) kupanga jinsi mmiliki wa leseni na chombo kingine kinachohusika na masuala ya dharura wanaweza kushirikiana kupunguza ajali kwa maisha au mali.

Majukumu na wajibu

85.-(1) Kila mmiliki wa leseni atafafanua majukumu na wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti wakati wa hali ya kawaida, hali isiyo ya kawaida na dharura.

(2) Kwa madhumuni ya kumuwezesha mwendeshaji

wa chumba cha udhibiti kuikabili kwa haraka na kwa usahihi hali ya uendeshaji, mmiliki wa leseni atafafanua kila kimoja kati ya vifuatavyo:

(a) mamlaka na wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti katika kufanya uamuzi na kuchukua hatua wakati wa shughuli za kawaida;

(b) wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti wakati hali isiyo ya kawaida ya uendeshaji inapogunduliwa, hata kama mwendeshaji wa chumba cha kudhibiti si wa kwanza kugundua hali hiyo, ikiwemo wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha kudhibiti kuchukua hatua mahsusi na kuwasiliana na wengine;

(c) wajibu wa mwendeshaji wa chumba cha kudhibiti wakati wa dharura, hata kama yeye si wa kwanza kugundua dharura, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua mahsusi na kuwasiliana na wengine;

(d) njia ya kuweka kumbukumbu za mwendeshaji wa chumba cha udhibiti kuhusu mabadiliko ya saa za kazi na kupokezana majukumu ya kazi kati ya waendeshaji wa chumba cha udhibiti au kutayarisha mfumo wa kuweka taarifa wakati mwendeshaji ana jukumu la kufuatilia au kudhibiti sehemu yeyote ya miundombinu ya umeme;

(e) majukumu, wajibu na sifa za watu wengine walio na mamlaka ya kuelekeza au kubadilisha hatua mahsusi za kiufundi za mwendeshaji wa chumba cha udhibiti;

(f) kuanzisha muda wa kufanya kazi kwa awamu, utaratibu wa kupokezana na kuanzisha kiwango cha juu cha saa za kutoa huduma ili kuhakikisha kuwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti wanaweza kupata saa nane za kulala wakati wa hali ya kawaida ya uendeshaji; na

(g) kuelimisha na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi husika kuhusu uchovu na namna ya kupunguza uchovu.

Taarifa inayotosheleza

86.-(1) Kila mmiliki wa leseni atawapatia waendeshaji wa chumba chake cha udhibiti taarifa, zana,

michakato na taratibu zinazohitajika kwa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti kutekeleza majukumu na wajibu.

(2) Mmiliki wa leseni atafafanua taratibu za mwendeshaji wa chumba cha udhibiti katika kutekeleza yafuatayo:

(a) kufanya tathimini ya kila sehemu kati ya picha za SCADA na vifaa husika nje ya chumba wakati vifaa hivyo vimejumuishwa au kuondolewa na wakati mabadiliko mengine yanayoathiri usalama wa miundombinu ya umeme yanafanywa kwa vifaa au picha za SCADA;

(b) kujaribu na kuhakiki mpango wa mawasiliano ya ndani ili kutoa nyenzo sahihi kwa ajili ya uendeshaji wa miundombinu ya umeme kwa usalama, angalau mara moja kila mwaka;

(c) kuhakiki mfumo dada wa SCADA angalau mara moja kwa mwaka; na

(d) kuanzisha na kutekeleza utaratibu wa kumwezesha mwendeshaji tofauti wa chumba cha udhibiti kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na aina ya taarifa ya kubadilishana.

Kuhimili uchovu

87. Mmiliki wa leseni atatekeleza njia zifuatazo ili kupunguza hatari inayohusiana na uchovu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ambao unaweza kuathiri uwezo wake wa kutekeleza majukumu na wajibu:

(a) kuanzisha muda wa kufanya kazikwa awamu na utaratibu wa kupokezana ambao utawezesha kupata muda wa kutokufanya kazi unaoruhusu angalau saa 8 za kulala;

(b) kuwaelimisha waendeshaji na wasimamizi wa vyumba vya udhibiti kuhusu mbinu za kuhimili uchovu na jinsi shughuli za nje ya kazi zinavyochangia uchovu;

(c) kutoa mafunzo kwa waendeshaji na wasimamizi wa vyumba vya udhibiti kutambua athari za uchovu; na

(d) kuweka ukomo wa juu wa saa za kazi kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti, ambao unaweza kukiukwa wakati wa dharura pale itakapolazimu, kwa uendeshaji salama wa kituo

cha miundombinu ya umeme.

Usimamizi wa kiashirio

88.-(1) Kila mwenye leseni anayetumia mfumo wa SCADA atakuwa na mpango ulioandikwa wa kushughulikia onyo la hatari ili mwendeshaji wa chumba cha udhibiti aweze kushughulikia kwa uhakika onyo la hatari.

(2) Mpango wa mmiliki wa leseni utajumuisha masharti ya-

(a) kuhakiki uendeshaji wa vifaa vya onyo la hatari vya SCADA kwa kutumia mfumo ambao unahakikisha vifaa hivyo viko sahihi na vinasaidia usalama katika shughuli za uendeshaji;

(b) kubaini angalau mara moja kwa mwezi sehemu zinazoathiri usalama ambazo zimeondolewa katika kuchunguzwa ndani ya mfumo wa SCADA, zimezuia vifaa vya onyo kutofanya kazi vizuri, zimesababisha milio ya onyo isiyo sahihi, au zimelazimisha matumizi ya mikono kwa saa nyingi zaidi ya zile zinazotakiwa katika kufanya matengenezo yanayotakiwa, au kufanya shughuli za uendeshaji;

(c) kuthibitisha usahihi wa eneo la kuweka viashiria vinavyohusiana na usalama na maelezo ya viashiria angalau mara moja kila mwaka;

(d) kukagua mpango wa usimamizi wa viashiria unaohitajika chini ya kanuni hii angalau mara moja kila mwaka ili kubaini ufanisi wa mpango huo;

(e) kufuatilia maudhui na kiasi cha shughuli za jumla zinazofanywa na kila mwendeshaji wa chumba cha udhibiti angalau mara moja kila mwaka, ambapo itahakikisha mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ana muda wa kutosha wa kuchanganua na kuitikia viashiria vinavyoita;

(f) Mmiliki wa leseni, kila mwaka-

(i) atajaribu na kuhakiki mpango wa mawasiliano wa ndani kwa ajili ya uendeshaji wa kituo kwa mikono; na

(ii) atajaribu mifumo dada yoyote ya SCADA.

Uhakiki wa

89.-(1) Mmiliki wa leseni atafanya tathimini ya kila

SCADA

sehemu kati ya picha za SCADA na vifaa husika nje ya chumba wakati vifaa hivyo vimejumuishwa au kuondolewa na wakati mabadiliko mengine yanayo athiri usalama wa miundombinu ya umeme yanafanywa kwa vifaa au picha za SCADA.

(2) Mmiliki wa leseni ataamua ni mabadiliko gani yatakayoathiri usalama wa kituo, na kufanya uhakiki kama itakavyohitajika kwa ajili ya marekebisho ya baadae ya mfumo.

Usimamizi wa mabadiliko

90. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa mabadiliko yanayoweza kuathiri shughuli za chumba cha udhibiti yanaratibiwa na wataalamu wa chumba cha udhibiti kwa kutekeleza yafuatayo:

(a) kuanzisha mawasiliano kati ya wawakilishi, wasimamizi na wataalamu wa shughuli zinazohusu chumba cha udhibiti wakati wa kupanga na kutekeleza mabadiliko ya nje kwa vifaa vya kituo;

(b) kuwataka wataalamu katika maeneo ya kazi kuwasiliana na chumba cha udhibiti kunapokuwa na hali za dharura na wakati wa kufanya mabadiliko katika eneo la kazi ambayo yanaathiri shughuli za chumba cha udhibiti; na

(c) kushirikisha chumba cha udhibiti au menejimenti ya chumba cha udhibiti kushiriki katika kupanga kabla ya kutekeleza mabadiliko makubwa.

Uzoefu wa uendeshaji

91. Mmiliki wa leseni atahakikisha kwamba mafunzo aliyojifunza kutokana na uzoefu wa uendeshaji yanajumuishwa, kadiri iwezekanavyo, katika utaratibu wake wa usimamizi wa chumba cha udhibiti kwa kufanya yafuatayo:

(a) kupitia matukio yaliyoripotiwa ili kubaini kama matendo ya chumba cha udhibiti yalichangia tukio lolote na, kama ni hivyo, kurekebisha, pale inapolazimu, mapungufu yaliyohusiana na-

(i) uchovu wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti;

(ii) vifaa vya maeneo ya kazi;

(iii)utendaji kazi wa kifaa chochote cha ulinzi;

(iv) utaratibu;

(v) usanifu wa mfumo wa SCADA; na

(vi) utendaji wa mfumo wa SCADA.

(b) kujumuisha mafunzo yaliyopatikana kutoka matendo bora kimataifa ya utoaji huduma.

Mpangilio wa chumba cha udhibiti

92. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa mpangilio wa chumba cha udhibiti una sifa zifuatazo:

(a) una nafasi ya kutosha kwa vipimo vya chumba cha udhibiti;

(b) unatokana na uchambuzi wa kazi zitakazo fanyika, kama uchambuzi wa kazi zinazohusiana au uchambuzi wa madaraja ya kazi;

(c) una njia za dharura za kutosha ambazo zinaweza kutumiwa na watokaji wanaofikia angalau asilimia 99;

(d) njia ya kuingia na ya kutoka inayozingatia waendeshaji wa vyumba vya udhibiti wenye ulemavu;

(e) unatumika mipangilio sawa pale ambapo kuna vyumba vingi vya udhibiti vinavyofanya kazi katika mfumo huohuo, ili kuhakikisha mfanano;

(f) viungo vyote vya uendeshaji kati ya waendeshaji wa chumba cha udhibiti vinazingatiwa wakati wa hatua ya usanifu;

(g) mawasiliano ya maneno na yasiyo ya maneno hayazuiliwi na mpangilio unapaswa kuwezesha kufanya kazi kwa pamoja;

(h) mpangilio wa chumba cha udhibiti unaonesha ugawaji wa majukumu na mahitaji ya usimamizi;

(i) mpangilio unakuwa wa ufanisi katika viwango vya juu na vya chini vya wafanyakazi;

(j) mzunguko wa wataalamu wote unafikiwa bila usumbufu kwa waendeshaji wa chumba cha udhibiti;

(k) pale ambapo nafasi za usimamizi zitaongeza kiasi cha mzunguko wa wataalamu, nafasi hizo zinawekwa karibu na milango mikubwa ya kuingilia;

(l) umbali kati ya vituo vya kazi unahakikisha kuwa waendeshaji wa vyumba vya udhibiti hawakai

kwa ukaribu;

(m) umbali wa chini wa nafasi kati ya vituo vya kazi utakuwa angalau milimita 3000;

(n) nafasi ya kutosha iwepoili uendeshaji mitambo bila kukusudia wakati wa kufanya matengenezo usiwezekane; na

(o) nyuma ya vifaa vya paneli kunawekewa alama kwa usahihi ili kupunguza uwezekano wa makosa ya kibinadamu.

Hali ya joto

93. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa hali ya joto na mzunguko wa hewa ya chumba cha udhibiti vinarekebika kwa viwango vinavyokubalika kwa kuzingatia Matendo Bora ya Utoaji Huduma.

Muonekano

94. Mmiliki wa leseni atahakikisha yafuatayo:

(a) mwanga wa taa kwenye chumba cha udhibiti hautakiwi kuweka vivuli katika vitengo vya kuonesha picha au sehemu nyingine inayong'aa ambayo inahitaji kufuatiliwa;

(b) mwanga wa taa katika chumba cha udhibiti uwe wa kiwango kati ya 500-800 *lux*;

(c) hakuna muonekano wa mwanga wa kuumiza utokanao na radi;

(d) madirisha kwenye chumba cha udhibiti hayasababishi vivuli katika sehemu zinazong'aa na hatua za kukinga mionzi ya jua zinachukuliwa.

Hali ya usikivu

95. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa-

(a) kiwango cha kelele katika chumba cha udhibiti kinarekodiwa na kisizidi 85 dB (A) kwa siku nzima ya kazi;

(b) kelele ya muda mrefu au kelele za masafa ya chini zaidi au ya juu zaidi zinaepukwa; na

(c) viwango vya kelele haviingilii mawasiliano, ishara za onyo na utendaji wa akili.

Kiashiria

96.-(1) Mmiliki wa leseni atahakikisha kwamba wafanyakazi na wakandarasi wote katika maeneo ya kazi wanajua maana ya kila kiashiria, mwitikio unaohitajika na ikiwa sababu ya kiashiria inaweza kuwaathiri.

(2) Kiashiria kitakuwa na uwezo wa kurudia chenyewe katika hali yake ya kawaida ikiwa hitilafu imerekebishwa.

(3) Ujumbe wa kiashiria utawasilishwa katika muundo mahsusi kulingana na kanuni zilizopo.

(4) Ujumbe wa kiashiria utamjulisha wazi mwendeshaji wa chumba cha udhibiti sababu ya kiashiria.

(5) Kufuatia kiashiria, mwitikio unaohitajika wa mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ni lazima uwe wazi.

(6) Utambulisho wa kiashiria haufai kutegemea rangi pekee, kwani waendeshaji wa vyumba vya udhibiti wenye upungufu katika utambuzi wa rangi hawataweza kutambua kinachoashiriwa na kiashiria.

(7) Ishara za kiashiria zitakuwa angalau kwa kiwango cha 10 dB (A) juu ya kelele za kawaida ndani ya chumba cha udhibiti.

(8) Kiashiria hakitazuia mawasiliano muhimu ndani ya chumba cha udhibiti.

(9) Rekodi ya kiashiria itatolewa kwa madhumuni ya uchunguzi.

(10) Muundo wa mfumo wa kiashiria utazuia sauti isitoke kwa wingi sana au sauti isitoke kwa kidogo sana ila itoke kwa wastani.

Lugha

97. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa lugha inayotumiwa mara zote ni rahisi kueleweka na mwendeshaji wa chumba cha udhibiti.

Lebo

98. Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa uwekaji lebo unatumika mara kwa mara kwenye mtambo wote na lebo-.

(a) zina uhusiano wa wazi na vifaa vinavyorejewa;

(a) zinasomeka kirahisi; na

(b) zinatumia vifupisho vinavyoeleweka kama matumizi ya vifupisho yanahitajika.

Vifaa vya kuonesha

99.-(1) Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa vifaa vya kuonesha vinafaa kwa aina ya taarifa vinavyowasilisha.

(2) Vifaa vya kuonesha vitapangwa kimantiki ili kuboresha utambuzi wa mawimbi.

(3) Mfuatano wa kazi na mbinu za uchanganuzi

zitatumika kwa lengo la kubaini mpangilio bora zaidi wa maonyesho na vidhibiti vinavyohusika.

(4) Uhusiano kati ya udhibiti na onesho lake linalohusika utakuwa dhahiri kama ifuatavyo:

(a) mwendeshaji wa chumba cha udhibiti ataelewa kwa urahisi matokeo ya onyesho;

(b) majibu ya matokeo yatakuwa wazi, pale inapowezekana; na

(c) njia ya udhibiti iliyotolewa kwa usogezaji katika maonyesho itafaa kwa kazi.

Uhakiki wa mazingatio

100. Mmiliki wa leseni atawasilisha utaratibu wake wa usimamizi wa chumba cha udhibiti kwa Mamlaka pale itakapohitajika.

Uzingatiaji na ukiukaji

101. Mmiliki wa leseni atatunza kwa ajili ya mapitio wakati wa ukaguzi-

(a) kumbukumbu zinazoonesha uzingatiaji wa matakwa ya Sehemu hii; na

(b) nyaraka za kuonesha kwamba ukiukaji wowote wa utaratibu unaohitajika na kifungu hiki ulikuwa muhimu kwa uendeshaji salama wa kituo.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

Mpango wa kuondoa miundombinu

102.-(1) Mmiliki wa leseni, ndani ya kipindi kisichopungua miezi sita kabla ya kumalizika kwa muda wa leseni na bila ya kuwepo kwa nyongeza yoyote ya muda wake au maombi ya kuhuisha au kuhamisha, atawasilisha kwa Mamlaka kwa ajili ya kuidhinishwa, mpango wa kuondoa miundombinu ya kituo chenye leseni ambao utajumuisha:

(a) ratiba ya kuvunjwa, kusafirisha tena nje ya nchi, kama ipo, na kuondoa masalia ya kituo chenye leseni; na

(b) taarifa ya mbinu ya kurejesha ardhi na mazingira katika hali yake ya asili na kwa kuziridhisha mamlaka zote zinazohusika.

(2) Mmiliki wa leseni, baada ya kuisha kwa muda wa leseni na bila ya kuwepo maombi yoyote ya kuhuishwa au

kuongezwa kwa muda wa leseni, atatekeleza mpango wa kuondoa miundiombinu ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Mmiliki wa leseni, endapo kituo chenye leseni hakitaondolewa kwa mujibu wa mpango wa kuondoa miundombinu kama inavyotakiwa katika kanuni ndogo ya (2), atawajibika kwa malipo ya tozo au adhabu yoyote ambayo inaweza kutolewa na mamlaka yoyote husika.

Kuondoa miundombinu leseni inapofutwa

103. Bila kujali masharti yaliyotangulia, mmiliki wa leseni ambae amefutiwa leseni na bila ya kuwepo kwa mmiliki wa leseni mwingine yeyote anayechukua shughuli ya kituo chenye leseni, ataondoa miundombinu ya uzalishaji kwa mujibu wa Matendo Bora ya Utoaji Huduma.

Makosa

104. Mtu ambaye anakiuka masharti ya kanuni hizi na hakuna adhabu mahsusi iliyowekwa anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.

Kufutwa TS. Na. 452 la 2023

105. Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme za Mwaka 2023 zinafutwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 74(1))*

FOMU YA MAOMBI YA KUTEULIWA KAMA MTEJA STAHIKI

| NA. | MAELEZO | SEHEMU HII IJAZWE NA MWOMBAJI |
|---|---|---|
| 1 | Maelezo ya Jumla | |
| | Jina la Mwombaji | |
| | Hati ya Usajili Na. (kama inahitajika) | |
| 2 | Anwani ya Makazi na ya Posta ya Mwombaji: | |
| | Anwani ya makazi: (Kiwanja Na., Nyumba Na., Mtaa) | |
| | Anwani ya Posta: | |
| | Kata / Nji | |
| | Wilaya | |
| | Mkoa | |
| | Simu: | |
| | Nukushi: | |
| | Simu ya mkononi: | |
| | Barua pepe: | |
| 3 | Jina la Msambazaji | |
| | Anwani ya Makazi: (Kiwanja Na., Nyumba Na., Mtaa) | |
| | Anwani ya Posta: | |
| | Leseni ya Umeme Na. | |
| | Tarehe ya Kuisha Muda wa Leseni: | |
| 4 | Vipimo vya Kiufundi | |
| | Kiwango cha juu cha Hitaji la Mwombaji (MW) | |
| | Volteji (kV) | |
| | | |
| 5 | Saini ya Mwombaji | |
| | Jina | |
| | Saini | |
| | Wadhifa | |
| | Tarehe | |

Dodoma,
……………, 2024

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*